# *NGUVU ZA MUNGU ZA KUGEUZA*

[Ndugu Branham anatambulishwa na Ndugu Carl Williams—Mh.] Asante, ndugu. [“Hakika imekuwa ni majaliwa kweli kumfanya Ndugu Branham aje Phoenix mara nyingi. Nafikiri yeye huja Phoenix kuliko mahali popote pale. Nasi tunamtaka aendelee kuja, mradi tu mimi niko huku, haidhuru. Mungu akubariki, Ndugu Branham.”] Asante, asante, Ndugu Williams.

Habari za asubuhi, marafiki. Mimi . . . Hawa wa familia ya Shakarian, Ndugu Williams na Dada Williams na wengi wao hapa wanajua habari zake. Niliona hilo katika ono, yapata miaka miwili hadi mitatu kabla hajakuwa mgonjwa, nalo likatukia.

2 Na mwaka uliopita tulipokuwa hapa, ninaamini ilikuwa ni Januari, kwenye ule mkutano, ilikuwa ni wakati ambapo yule kasisi (jina lake ni nani? Ninasahau jina lake sasa) alipokuwa hapa. [Mtu fulani anasema, “Stanley.”—Mh.] Stanley, Askofu Stanley, kutoka kanisa Katoliki. Mnakumbuka ule wakati aliponiletea ile Biblia, mwajua, naye akaniambia.

Wengi walikuwa wakitabiri, “Binti yangu, umeponywa.”

3 Naye alijua ya kwamba lile ono lilikuwa limesema ya kwamba asingepona. “Angekufa kati ya saa nane na saa tisa usiku.” Mnakumbuka hilo? [Mtu fulani anasema, “Naam.”—Mh.] Kwa hiyo, saa nane ama saa tisa.

4 Nami nisingeweza kumwambia Demos. Na hata hivyo nilimwambia mama yake wa kambo, moja kwa moja mle chumbani, ng’ambo ya pili ya mahali hapa. Nikasema, “Hatapona.”

Bibi Shakarian akasema, “Vema, kila mtu anatabiri.”

5 Nikasema, “Hakika, ningeweza kukosea, mimi mwenyewe, bali nilisema. Yeye hatapona.”

6 Niliwaambia wengi wao, yapata miaka mitatu iliyopita, “Nilimwona akiyakimbilia maisha yake, naye akaingia kitandani. Kisha akainua mikono yake na kunipigia makelele, namna hiyo. Nami hata ni—nisingeweza kumfikia. Ndipo nikamwona akifa. Nami nikaangalia, na palikuwapo na kitu fulani, palikuwapo na saa ya ukutani, nayo ikasema ni kitu fulani kati ya saa nane na saa tisa.”

7 Na kwa hiyo huyo askofu akasema, “Vema, nitaangalia tu nione jinsi hilo litakavyotimia.” Kwa hiyo, kweli lilitimia.

8 Hakika tunasikitika. Ninajisikia kanisa limempoteza mtu mashuhuri, katika Dada Florence Shakarian. Lakini, yeye

alikuwa ni mwimbaji hodari, alikuwa ni mwanamke aliyejazwa na Roho.

9 Nilikuwa pamoja na mama yake; mama yake alikuwa ni mmoja wa wahusika wangu wa kwanza niliokuwa nao kwenye Pwani ya Magharibi, wakati mama yake alipoponywa. Wakati madaktari. . . Alikuwa amepoteza fahamu, na amevimba sana. Na kwa hiyo yu—yule daktari aliyekuwa pale akaniambia, kasema, "Sasa kuwa mtulivu sana unapoomba. Usipige kelele nyingi. Mwanamke huyo yuafa."

Nikasema, "Naam, bwana."

10 Naye akasema, basi, akaendelea tu kuniambia. Na, vema, hata sikupata nafasi ya kuufungua mdomo wangu, kitu kama hicho.

11 Kwa hiyo, Ndugu Demos ndiye aliyeniambia nipande niende nikamwone.

12 Kwa hiyo, nikapanda orofa ya juu. Naye Florence alikuwa amepiga magoti sakafuni, wakati huo akiwa ni msichana mdogo mrembo, na wanawake wengine. Ndipo nikaenda pale nikamwombea, na kulisema. Naye alikuwa amepoteza fahamu. Nami nikamwambia angeamka tena. Naye akaamka. Miaka kadhaa baadaye, akafa. Na sasa Mungu huyajibu maombi yetu.

13 Nasi tunajua hilo, tunaamini ya kwamba sote tumekuja hapa kwa mapenzi ya Mungu, na tunaondoka vivyo hivyo. Mmoja mmoja, kila mmoja wetu atavuka lile lango. Na hiyo ndiyo sababu tupo hapa asubuhi ya leo, tumekusanyika pamoja katika Ushirika huu wa Wafanyabiashara Wakristo, ni kuzungumza juu ya mambo haya, na kujiandaa kwa ajili ya hayo, maana tunajua hayana budi kutokea.

14 Sasa Dada Florence ni mwanamke mdogo, mwenye umri wa miaka arobaini na mbili, ndiyo kwanza Ndugu Williams aniambie, na ni mdogo sana. Lakini kabla wao, yeye alijua alikuwa na ugonjwa huu, mbona, niliona ono lake na likaniambia matokeo yake. Halafu, ingekuwa. Mungu anajua yote kuhusiana nalo, na yeye kumwona Yesu chumbani mwake kabla hajatuacha. Hatutaki tu kumwombea, kwa kuwa tumefanya hivyo sana. Tunataka tu kumshukuru Mungu kwa ajili ya maisha yaliyokuwa miongoni mwetu, yaliyotuvutia sisi sote, kama Dada Shakarian.

15 Nasi tunataka kumwombea Ndugu Demos, Dada Rose. Na kumbukeni, wamekuwa na pigo kubwa mno maishani mwao, katika ninii ya mwisho. . . ni baba yake, na dada yake sasa katika ninii yake. . . miaka ya mwisho. [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Lakini, na, naam, chini ya, chini, miezi kumi; na dada, Dada Edna, pia.

16 Kwa hiyo, ninajua jinsi ya kumhurumia Ndugu Demos. Nilikuwa na baba, ndugu, mke, na mtoto mchanga walioaga

dunia wakiachana kwa siku chache, kwa hiyo ni—ninajua jinsi anavyojisikia asubuhi ya leo. Unajua tu wakati umepitia hayo, hapo ndipo unapojua jinsi ya kuhurumia. Na . . .

17 [Vipaza sauti vinalia—Mh.] Nilifanya hilo mwenyewe. Samahani. Niligonga kidude kidogo mahali fulani hapa, kwa mkono wangu. Kwa hiyo ni—nasikitika nilivifanya vitoe sauti kubwa mno, pasipo kukusudia.

18 Kwa hiyo hebu na tusimame sasa wakati tukininii . . . mkiweza, kama ni ninii . . . Na tuinamishe kichwa chetu.

19 Baba wa Mbinguni, tumekusanyika hapa asubuhi ya leo kukuabudu Wewe, na kukushukuru na kukusifu, kwa kututumia Yesu Mkombozi wetu, hata tuna tumaini baada ya maisha haya kwisha, kwa kuwa tunaona ya kwamba haijulikani kama tutaishi hapa wakati wote. Na, Baba, kuona hali za kutisha miili hii inazoweza kufikia, tunashukuru haitubidi kukaa hapa wakati wote. Wewe umeandaa njia ya kuepukia, kupitia kwenye bonde la mauti.

20 Na, Baba, tunakushukuru asubuhi ya leo, kwa ajili ya maisha ya mmoja aliyesimama pamoja nasi, chini ya mwaka mmoja uliopita, akiimba sifa Zako; Dada Florence Shakarian, jinsi tulivyomfahamu. Nawe umetwambia muda mrefu kabla, hata miaka, ya kwamba jambo hili lilikuwa linaenda kutukia, kusudi lisitushitue sana. Nasi tunajua ya kwamba unayosema ni kweli. Halafu Neno Lako linasema, "Mtu aliyezaliwa na mwanamke, amejaa siku chache na amejaa taabu." Tunajua hiyo ni kweli, pia, Bwana. Tunajua sote hatuna budi kupitia kwenye bonde hilo. Kwa hiyo tunakushukuru kwa ajili ya maisha yake yaliyokuwa humu duniani. Na tukiamini kwa imani, kwamba sasa, asubuhi ya leo, yeye amepita kutoka kwenye nyumba hii ya wadudu yenye mashaka, akaingia kwenye mwili wenye utukufu ambao kamwe hauwezi kuugua. Na kipaji chake cha kuimba, na sauti aliyokuwa nayo, na roho yake imejaa neema sana pamoja na Kristo! Kwamba angeweza kurudi asubuhi ya leo, asingerudi kwa vyovyote kamwe; ingembidi kupitia haya yote tena. Ambayo, sasa yamekwisha, yeye yuko pamoja na mama yake na baba yake. Walimwita mtoto wao mchanga aende nyumbani. Kwa hiyo, tu—tunakushukuru.

21 Pia tunataka kuombea faraja, kwa ajili ya Ndugu yetu Shakarian, ndugu yetu mpendwa, tukijua ma—maisha ambayo ameishi, na mateso anayopitia katika siku hizi za mwisho, na jinsi alivyo; tunamwona akizeeka, na nywele zake zikiisha, na mabega yake yakiinama, na hata hivyo akijaribu kukaa hudumani kwa ajili ya Mungu. Mungu, mpe nguvu leo. Tunaomba, Mungu, ya kwamba utamjalia. Kwa wote wale wanaoomboleza kuondoka kwake, tunamwombea kila mmoja.

22 Na tujalie, Bwana, tunapowazia juu ya hili, tukumbuke ya kwamba sisi nasi hatuna budi kuondoka siku moja.

Wakati tumeketi pamoja hapa katika Uwepo wa Bwana Yesu, tungeomba kwamba ungetukumbusha jambo hili. Na jalia tujichunguze, kama tusemavyo, ama tufanye hesabu ya maisha yetu wenyewe, kwamba tuko chini ya Damu na katika Imani. Tujalie, Bwana.

23 Sasa wakati nikijaribu chini ya hali hizi kuuleta ujumbe mdogo kwa watu, leo, ninaomba ya kwamba Wewe utanisaidia, Bwana. Nipe nguvu, kwa kuwa ni—ni—ninazihitaji, Bwana. Nami ninaomba ya kwamba utatujalia. Na jalia jambo fulani lisemwe ambalo lingekuadhimisha tu. Na kukiwapo na yeyote chini ya mlio wa sauti yetu asubuhi hii, ambaye hayuko tayari kukabiliana na saa iliyowekwa mbele zao, jalia huu uwe ndio wakati ambapo watajisalimisha Kwake Yeye aliyesema, "Mimi Ndimi Njia, Uzima, Kweli," yaani Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina. (Mwaweza kuketi.)

24 [Mtu fulani jukwaani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ndugu hapa anataka kujua kama kila mtu anaweza kusikia vema. Ana maikrofoni mbili zilizowashwa. Hiyo ni sawa? Mnaweza kusikia? Inueni mikono yenu kama mnaweza. Mnaweza kusikia? Inueni mikono yenu. Vema.

25 Nasikitika ya kwamba hatuna nafasi ya kila mtu kuketi asubuhi ya leo. Nasi tunatumaini ya kwamba sitakaa hapa muda mrefu kupita kiasi, wa kutosha tu labda kutuletea labda somo la Neno; kwamba Bwana Mungu ataliheshimu Neno Lake ambalo linasomwa, Naye atatupa neema Yake, tupate kumtumikia kwake.

26 Sasa niliambiwa na Billy Paul, asubuhi ya leo, ya kwamba huenda ikawezekana kwamba tutahubiri Jumapili ijayo kwenye Assembly of God ya Grantway, huko Tucson. Kama kuna mtu yeyote hapa kutoka Tucson, huenda nisikuone juma hili. Nitakuwa kwenye Assembly of God ya Grantway, Jumapili ijayo.

27 Kwa hiyo sasa ndio kwanza turudi kutoka huko Mashariki, na kwa namna fulani nilijichosha kidogo, kwa kula kupita kiasi, kwa ukarimu uliopitiliza wa watu huko chini milimani. Na—nami nikawa mgonjwa, kwa hiyo sijajisikia vizuri juma hili. Kwa hiyo, niombeeni. Na . . .

28 [Mtu fulani anasema, "Oposamu nyingi kupita kiasi."—Mh.] Ati umesema nini? ["Oposamu nyingi kupita kiasi."] Ndugu Carl Williams na ucheshi wake, nami nafikiri tunauhitaji sasa hivi, yeye alisema, "Oposamu nyingi kupita kiasi." Sijui juu ya hilo, Ndugu Carl, bali kuchakulo wengi mno. [Ndugu Branham anacheka.]

29 Kwa hiyo ukitaka kumwombea mtu fulani asubuhi ya leo, mbona, ha—hakika ninayathamini kama yangekuwa ni baadhi ya maombi yenu kwa ajili yangu, kwa kuwa na—nayahitaji.

Sasa tunataka kuingia upesi kwenye Neno.

30 Nami sitaki kuwaweka hapa kwa muda mrefu kupita kiasi, kwa maana ninaamini kuna muunganisho wa simu kote nchini, juu ya huu asubuhi ya leo, unaenda kote kutoka kwenye Pwani ya Magharibi hadi Pwani ya Mashariki, kutoka Kaskazini hadi Kusini. Mashirika mengi, mengi sana yameshirikishwa kama vile ninyi nyote mlivyoshirikishwa hapa kutoka maskanini. Pia imeunganishwa huko Phoenix, hiyo ni kila mahali palipo na ibada, yanakuja moja kwa moja kwenye. . . Nao wanakusanyika katika makanisa na majumbani, na vitu kama hivyo, kupitia kwenye wimbi zuri sana. Wanasema hata ni zuri kuliko matangazo. Ni muunganisho wa simu, wanaweka kipokezi ama maikrofoni, ama chochote kile, chumbani. Nao. . . Mke wangu alisema, akitoka Indiana juma lililopita, akishuka kuja Tucson, ilikuwa ni kama tu kusimama humu chumbani. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba Mungu atawabariki wale wote walio kwenye mtandao huu asubuhi ya leo, popote walipo. Huko juu New York sasa itakuwa, loo, alasiri, na nyakati mbalimbali unapoivuka nchi.

31 Sasa kwenye Kitabu cha Warumi, mlango wa 12, na kifungu cha kwanza na cha pili, tunataka—tunataka kusoma Andiko hili.

> *Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.*
>
> *Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema na* makamilifu. . . mema, *mapenzi ya Mungu yanayompendeza, na makamilifu.*

32 Sasa, Bwana akipenda, ninataka kuchukua somo langu kwa ajili ya asubuhi ya leo, juu ya: *Nguvu Za Mungu Za Kugeuza.*

> Kusudi *msiifuatishe namna ya dunia hii; bali. . . mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu,* sasa, na mjue hakika *yale mapenzi ya Mungu yaliyo mema,* makamilifu, yanayompendeza.

33 Ni fungu la maneno linalojulikana ambalo wengi wa wachungaji wenu wamelitumia kote katika wakati wenu. Limetumiwa tangu lilipoandikwa. Lakini hata hivyo, jambo moja kuhusu Neno la Mungu, kamwe halizeeki, kwa kuwa ni Mungu. Halizeeki kamwe. Kupitia kwenye kila kizazi sasa, karibu sana, yapata miaka elfu mbili na mia nane, ama zaidi, Neno hili la Mungu limesomwa na wanadamu, makuhani, na kadhalika, wala halizeeki. Nimekuwa nikilisoma, mimi mwenyewe, kwa yapata miaka thelathini na mitano. Na kila ninapolisoma, ninapata kitu kipya ambacho sikukiona mara ya kwanza. Kwa sababu, limevuviwa, ni Mungu katika umbo la

barua. Mnaona, ni sifa za Mungu zikinena, nazo zimewekwa kwenye karatasi.

34 Mara nyingi, mwanadamu alisema, "Vema, sasa, mwanadamu aliiandika Biblia hii." La. Biblia inasema, Yenyewe, ya kwamba Mungu aliiandika Biblia. Ni Neno la Mungu.

35 Wala kamwe haliwezi kushindwa. Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitashindwa, zitapita, bali Maneno Yangu hayatashindwa kamwe." Wala haliwezi kushindwa, nalo ni Mungu, kwa sababu ni sehemu Yake.

36 Halafu wewe ukiwa ni mwanaye na bintiye, u sehemu Yake, na hiyo inakufanya kuwa ni sehemu Yake. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu sisi huja kushirki pamoja kwenye Neno la Mungu.

37 Sasa neno hili *kugeuzwa*, nililiangalia kwenye kamusi, jana. Wakati, karibu nishindwe kuuhesabu wakati niliopaswa kuwa huku juu, nilipokuwa nikilitafuta somo, nami nikalipata neno hili, ama fungu hili, hasa, Andiko. Na kwenye kamusi inasema ya kwamba ni "kitu kilichobadilika." Ni "kubadilika." *Kugeuza*, "kufanywa tofauti na ilivyokuwa." Imekuwa, "Tabia yake na kila kitu ndani yake kimebadilishwa," *kugeuza*.

38 Nami nikiwazia asubuhi ya leo, katika Mwanzo 1. Ulimwengu huu haukuwa na umbo, na ulikuwa tupu, na giza lilikuwa juu ya nchi; si kitu ila mchafuko mtupu. Basi wakati ulimwengu huu ulipokuwa katika hali hiyo, Roho ya Mungu ilitulia juu ya uso wa maji, ndipo hiyo picha nzima ikabadilika; kutoka kwenye mchafuko mtupu, ikawa ni bustani ya Edeni. Hizo ni Nguvu za Mungu za kugeuza, ambazo zinaweza kuchukua kitu kilicho bure na kufanya kitu cha ajabu kutoka kwake. Nguvu za Mungu za kugeuza!

39 Nasi tunafahamu kwamba, kwa kuyasoma Maandiko, ya kwamba Mungu alichukua miaka elfu si—sita katika kufanya maandalizi kwa ajili ya Edeni hii. Sasa, huenda hakuchukua muda mrefu jinsi hiyo; bali ni kudhania tu, na kulichukulia kwenye Maandiko ambapo yalisema "siku moja kwa Mungu, ni miaka elfu moja duniani," hiyo ni kusema, kama Mungu angeuhesabu wakati. Na tuseme alichukua miaka elfu sita katika kuifanya dunia, Naye alikuwa amepanda duniani mbegu zote nzuri. Kila kitu kilikuwa tu ni kikamilifu.

40 Nafikiri, mara nyingi, wakati hata wakosoaji wanapoanza kusoma Kitabu cha Mwanzo, wanaanza kukikosoa, kwa kuwa inaonekana kana kwamba daima kinajirudia, ama kinakurusha-rusha hapa na pale.

41 Lakini kama tungeangalia tu kwa dakika moja, kabla hatujaingilia somo letu, kwamba, Musa aliona ono. Naye Mungu akasema naye. Mungu alinena na Musa uso kwa uso, mdomo kwa sikio. Sasa, kamwe hakunena na mtu mwingine yeyote jinsi hiyo, kama alivyonena na Musa. Sasa, Musa alikuwa ni mtu mashuhuri, mmoja wa manabii walio wakuu sana. Yeye alikuwa

ni mfano wa Kristo. Na sasa Mungu anaweza kunena, Yeye ana sauti. Imesikiwa. Mungu anaweza kunena.

42 Pia Mungu anaweza kuandika. Mungu aliandika zile Amri kumi kwa kidole Chake Mwenyewe. Aliandika kwenye kuta za—za Babeli wakati mmoja, kwa kidole Chake. Aliinama chini na kuandika katika mchanga wakati mmoja, kwa kidole Chake. Mungu anaweza kunena. Mungu anaweza kusoma. Mungu anaweza kuandika.

43 Mungu ni Kisima cha neema yote na Nguvu, na hekima yote ya Kiungu, iko katika Mungu. Kwa hiyo basi, tukijua jambo hilo, Yeye Ndiye Muumba pekee aliyeko. Hakuna Muumba mwingine ila Mungu. Shetani hawezi kuumba, hata kidogo, yeye hupotosha tu kile kilichoumbwa. Lakini Mungu Ndiye Muumba pekee.

44 Kwa hiyo, Yeye aliumba kwa Neno Lake. Alilituma Neno Lake. Kwa hiyo mbegu zote alizokuwa ameweka ardhini, Yeye aliziumba mbegu hizo kwa Neno Lake Mwenyewe, kwa kuwa hapakuwapo na kitu kingine cha kufanyiza mbegu hizo. Yeye alikuwa ameziweka, nazo zilikuwa chini ya maji. Yeye alisema tu, "Na *hiki* kiwepo, na *kile* kiwepo."

45 Sasa tunaona ya kwamba, mara nyingi, inaonekana kana kwamba Biblia inajirudia ama kusema kitu ambacho haisemi. Kwa mfano, katika Mwanzo 1 tunaona ya kwamba, "Mungu alimuumba mtu kwa Mfano Wake Mwenyewe, kwa mfano wa Mungu alimwumba; mwanamume na mwanamke aliwaumba." Kisha anaendelea, na mambo mengi yakatukia juu ya nchi.

46 Ndipo tunakuja kuona, hapakuwapo na mtu wa kulima ardhi. "Basi Mungu akamwumba mtu kwa mavumbi ya ardhi." Huyo alikuwa ni mtu tofauti. "Naye akampulizia roho wa uhai ndani yake, naye akawa nafsi hai."

47 Mtu wa kwanza alikuwa katika mfano wa Mungu, ambao ni Roho. Yohana 4, inasema, "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo hawana budi kumwabudu katika Roho na katika Kweli." Lakini Mungu ni Roho. Naye mtu wa kwanza, ambaye Yeye alimwumba, alikuwa ni mtu-roho, naye alikuwa katika mfano na sura ya Mungu.

48 Ndipo akamweka mtu huyu katika mwili, kisha mtu akaanguka. Kwa hiyo basi Mungu akashuka na akawa katika mfano wa mwanadamu, apate kumkomboa mtu huyo aliyeanguka. Hiyo ndiyo hadithi halisi ya Injili, ni—nionavyo mimi.

49 Sasa, Mungu, katika miaka elfu sita, alikuwa amepanda mbegu hizi zote nzuri sana, ama alikuwa amenena Neno Lake. "Itakuwa *hivi*. Mti *huu* utakuwa. *Huu* utakuwa." Kila kitu kilikuwa ni kikamilifu. Kilikuwa ni kizuri tu. Naye akaamuru kila moja ya mbegu hizo kwamba zingekuwa, zingejigeuza ziwe mmea wa aina ya uhai ambao Neno la Mungu lilikuwa limenena

ndani yazo zitakuwa. Kama ulikuwa ni mwaloni, ulipaswa kuzaa mwaloni. Kama ulikuwa ni mtende, ulipaswa uzae mtende.

50 Kwa sababu, yule Muumba mkuu alikuwa ndiyo kwanza alitume Neno Lake, nayo mbegu Neno ilikuwa mle kabla ile mbegu halisi haijafanywa. Ndipo Neno likaifanya hiyo mbegu. Mnaona, "Yeye aliufanya ulimwengu kwa vitu visivyoonekana." Mnaona, Yeye—Yeye aliufanya ulimwengu kwa Neno Lake. Mungu alinena kila kitu kikawa.

51 Na akiwa ni Mungu, Muumba, akivinena vitu vyote vikawa, hapana shaka ulikuwa ni ulimwengu mkamilifu. Palikuwa ni mahali pa—pazuri. Ilikuwa ni paradiso ha—halisi kweli hapa duniani.

52 Sasa, kama, kila mahali hapana budi pawe na makao makuu mahali fulani. Mkutano huu una makao makuu, na tawi hili lina makao makuu, na kanisa lina makao makuu. Naye Mungu anayo makao makuu. Na kwa hiyo mahali hapa pakuu, taifa tunaloishi, lina makao makuu. Na kwa hiyo Edeni hii kuu ilikuwa na makao makuu, nayo makao yake makuu yalikuwa kwenye bustani ya Edeni, ama katika Edeni, mashariki mwa bustani hiyo.

53 Naye Mungu alimweka Mwanawe na bibi-arusi wa mwanawe, Adamu na Hawa, juu ya haya yote, wautawale uumbaji Wake wote mkuu hapa duniani.

54 Mungu alikuwa Baba wa Adamu. "Adamu alikuwa nanii . . . mwana wa Mungu," kulingana na Maandiko. Alikuwa ni mwana wa Mungu.

55 Ndipo Mungu akamfanyia msaidizi, kutoka mwilini mwake mwenyewe; labda ubavu kutoka juu ya moyo wake, apate kuwa karibu naye, ndipo akamfanyia msaidizi. Kwa kweli yeye hakuwa ni mke wake bado, si zaidi ya vile alivyokuwa mwanamume bado; Yeye alikuwa tu amelinena. Na hapo ndipo shida inapoingilia, Shetani alimpata kabla Adamu hajampata. Kwa hiyo, lilikuwa tu ni Neno Lake alilokuwa amelinena.

56 Ninasema kwamba, sitaki kutumia wakati mwingi kupita kiasi juu yake. Lakini baadhi yenu huenda kidogo mkachanganyikiwa, hasa sana baadhi ya watu huko—huko Kusini, inaonekana wanaona hili kidogo linatatanisha, juu ya Ujumbe nilio nao kutoka kwa Mungu leo hii, kwa watu, kuhusu uzao wa nyoka. Nami nitaenda nyumbani, Bwana akipenda, moja ya siku hizi, huko Jeffersonville. Ninataka yapata ujumbe wa saa sita, na kuyanyosha hayo kabisa, mnaona, kwa hiyo litaliweka kwa namna ambayo mtajua tunachozungumzia. Nayo ni BWANA ASEMA HIVI. Ni la kweli tu kama lilivyokuwa wakati lilipomwona Dada yetu Florence kabla hajatuacha, miaka kadhaa. Mnaona, ni Kweli. Na sasa, sisi, labda linaeleweka vibaya.

57 Kama mtu fulani angenijia, kitu fulani kinyume, kwa namna fulani ningekielewa vibaya, mimi mwenyewe. Nisingetaka

kukosoa yale mtu yeyote anayosema. Haitupasi kukosoana. Sina hatia ya kufanya hilo; ninamshukuru Mungu. Nimekosoa dhambi na kutokuamini; bali sio mtu binafsi, mnaona, si—sikosoi. Sisi—sisi ni ndugu na dada, tukijitahidi, tunashuka kuja mahali ambapo Dada Florence alifikia jana asubuhi, mnaona. Yeye, sisi, sote hatuna budi kuja hivyo. Wala silo kusudi langu ku—kujaribu kumkosoa ndugu ama dada ambaye asingekubaliana nawe. La, na iwe mbali nami kufanya hivyo! Sidhani kamwe mtapata kanda ambapo nilitaja jina la mtu yeyote. Ambapo, nimejisikia mara nyingi mtu huyo amekosea, bali hiyo ni kati yao na Mungu. Lakini makosa, kwa njia ya dhambi na. . . Na kutokuelewana wakati mwingine hata si dhambi, ni kutokuelewa tu kwa watu. Nami na—nafikiri kila mmoja wetu ana haki ya kujieleza mwenyewe tupate kufahamu.

58 Sasa Muumba huyu mkuu alikuwa amemweka mwanaye aliyeumbwa. Sasa, Adamu alikuwa ndiye mwanawe wa kwanza aliyeumbwa. Yesu alikuwa ndiye Mwanaye wa pekee *wa kuzaliwa*, mnaona, Yeye alizaliwa na mwanamke. Lakini Adamu alitoka moja kwa moja mkononi mwa Mungu, katika uumbaji.

59 Sasa makao makuu, pamoja na mwa—mwanawe na bibi-arusi wa Mwanawe wakiwa na mamlaka juu ya yote, yalionekana makamilifu kabisa. Kulikuwako na mwa—mwanamume, kiongozi wa hayo yote, mwanawe Mwenyewe pamoja na bibi-arusi wake.

60 Na kila mbegu ilikuwa ni kamilifu, mitende, na mialoni, na nyasi, na ndege, na wanyama. Na kila kitu kilikuwa katika utaratibu mkamilifu pamoja na Amri ya Mungu, "Usibadilishe tabia yako. Izae kwa jinsi yake, kila mbegu! Mwaloni, kamwe usipotoshwe ukawa mpaipai." Mnaona? "Mtende, usipotoshwe ukawa kitu kingine. Lakini kila mbegu kwa jinsi yake!" Naye alikuwa—alikuwa ameichunguza kote katika nyakati.

61 Naye alikuwa amelinena Neno. Nazo Nguvu Zake kuu za uumbaji zilikuwa zimevifanya vitu hivi vilivyotokea, na hata mwanamume na mwanamke. Nao walikuwa ni viongozi kwa sababu walikuwa ninii. . . walikuwa ni wakuu sana kwa jamii zingine zote. Naye akawaweka chini ya ulinzi wa kitu kile kile alioiweka miti, wanyama, na kadhalika: Neno Lake. Hawapaswi kamwe kabisa, kwa vyovyote vile, kulivunja Neno hilo. Hawana budi kudumu Mle. "Kamwe msiondoe chochote kutoka Kwake, wala kuongeza chochote Kwake! Inawapasa kuishi kwa Neno hili."

62 Na mradi tu uumbaji huo ungaliishi namna hiyo, isingalimbidi Dada Shakarian kuondoka asubuhi ya leo, mradi tu ungalidumu namna hiyo, uchumi mkuu wa Mungu! Ndiko tunaamini tunarudi. Tunarudi pale, mahali pale.

63 Ambapo hiyo asubuhi ya saba, wakati Mungu alipoyaangalia hayo yote, Naye alisema, "Ni mazuri. Ya—yananifurahisha.

Naam, ni—ni—nina furaha nilifanya hivyo. Na yote sasa yako chini ya udhibiti. Nami ninamwamini Mwanangu na mkewe, ya kwamba—ya kwamba wataninii (kuwafanya watawala wa hayo yote), kwamba watayaangalia yote na kuhakikisha ni sawa, kwamba kila kitu kitazaa kwa jinsi yake. Sasa yeye ana mamlaka ya kufanya hivyo." Mungu basi akasema, "Vema, ikiwa yote ni mazuri sana, na hayawezi kuwa vinginevyo, kwa kuwa ni mapenzi Yangu Mwenyewe. Ndivyo ninavyoyataka. Nami nimeyanena jinsi hiyo, na Maneno Yangu yameyaleta jinsi nilivyoyataka hasa. Na hayo hapo. Yote ni mazuri!" Kwa hiyo Biblia ilisema, "Mungu akapumzika siku ya saba, kutoka kazi Zake zote."

64 Na kila kitu chini ya udhibiti, kuzaa kwa jinsi yake. Sasa kumbuka, "kuzaa." Wakati Yeye alipoiweka mbegu ardhini, hiyo mbegu inaweza tu kuchipuka kwa nguvu za uhai ulio ndani yake, kuigeuza kutoka kwenye mbegu iwe mmea, ama chochote ilichokuwa. Nguvu Zake za kugeuza! Sasa, Mungu aliweka mbegu mle ndani, ikiwa na nguvu za uwezekano kwamba ingekuwa kile Yeye alisema itakuwa. Na mradi tu ilikaa katika mazingira yafaayo, ingekuwa kile hasa Mungu alichosema ingekuwa. Ilibidi iwe hivyo, kwa kuwa Yeye alikuwa ameifanya jinsi hiyo, na akafanya njia. Kwamba, kitu chochote kinachokaa kwenye njia Yake, kwenye mstari Wake wa Neno, hakina budi kuzaa kile hasa Neno Lake lilichosema kingezaa. Hakiwezi kutoka hapo. Kimeelekezwa vizuri kabisa. Kwa hiyo, kila kitu kikiwa kimetumainishwa kwa Mwanawe Mwenyewe, kwamba ingekuwa hivyo, basi Mungu akasema, "Yote ni mema, kwa hiyo nitapumzika tu. Na kila moja ya mbegu hizo ina nguvu ndani yake, kujigeuza yenyewe kuwa spishi ninayotaka iwe. Hivyo ndivyo haina budi kuwa, kwa sababu nimeipa kila mbegu nguvu za kujigeuza, kujifanya yenyewe, katika nguvu zake tendaji sasa kujifanya kile hasa ninachoitaka kuwa."

65 Mungu hajabadilika kamwe. Ni yeye yule leo tu kama alivyopata kuwa wakati huo! Mungu amekusudia kufanya jambo fulani. Yeye atalifanya. Hakuna kitu kitakachomkomesha. Atalifanya!

66 Sasa baada ya yote kuwekwa vizuri sana katika utaratibu, Mungu alijisikia hakika sasa kwamba hii ingekuwa ni sawa, ndipo basi, wakati alipofanya hivyo, ndipo adui akaingia. Nitaninii... Mungu alitoa nguvu za kugeuza. Nami nitamwita jamaa huyu, akiwa na nguvu sio—sio za kuumba tena, bali nitaninii... Yeye alikuwa na nguvu za kuumbua, sio kugeuza; bali kuumbua. Sasa, chochote kilichoumbuka kimetolewa kwenye hali yake asilia, kimeingiwa na kasoro fulani.

67 Miaka kadhaa iliyopita, kwenye doria, nikipitia mashamba ya mahindi, ningewazia, palikuwa na tawi lililong'oka mtini, likaangukia shina la mhindi. Nalo hilo shina lilikuwa likijaribu lilivyoweza kusimama wima kama lilivyopaswa kuwa, bali

lilikuwa limeumbuka kwa kuwa jambo fulani lilikuwa limetukia. Na kijiti hicho kilikuwa kimelilalia.

68 Ndipo tunaona mmea mwitu utambaao kondeni. Ambao, wengi wenu wanaume hapa, na labda baadhi yenu wanawake . . . kama mnatoka Kentucky. Wanawake wanatumia jembe kule kama vile mwanamume, anaenda shambani na je—jembe, tunaloita maskini jembe shingobata, na kukata vi—vitambaaji hivyo. Kwa maana, kama hukukatilia mbali vitambaaji hivyo, ambapo mahindi yalikuwa kwenye safu, namna *hii*, basi kitambaaji hicho kingetambaa, kiushike mhindi huo, na kujizungusha polepole, kwa urahisi mno, kijanja sana, hata usingeweza kujua kilikuwa kikijizungushia. Na hatimaye kinapata nguvu zaidi na zaidi, nacho kinauvuta mhindi huo mpaka unaumbuka. Kinaukumbatia, kinajizungushia kwenye shina lake lenyewe; kinauumbua kutokana na vile ulivyokuwa, ukawa kitu kingine. Hata hivyo ni mhindi, bali ni mhindi ulioumbuka.

69 Nasi sote tungali katika mfano wa Mungu. Lakini wengine wameumbuka sana, kama wana wa Mungu, wanaotembea kinyume na Neno Lake na kwa njia a—ambayo alituandalia na kutuwekea tuiendee. Tukiweka kitu fulani, ulimwengu unatupeleka kombo, unatuvuta karibu nao, na mbali na mstari huo mwembamba na ulionyoka, aliotupandia mle, tupate kuwa wana na binti za Mungu. Dhambi imefanya jambo hili ovu kwa wana na binti za Mungu.

70 Muumbuaji! Ninajua hili kidogo linaonekana la kigeni kulizungumzia jinsi hii, "ku—kuumbua," bali hivyo ndivyo alivyokuwa; aliumbua, ama akapotosha. *Kupotosha* maana yake ni "kubadilisha, kufanya kitu tofauti." Na *kuumbua* ni jambo lile lile, kwamba kimeletwa na kuumbuliwa, na "kufanyizwa vinginevyo." Hata hivyo ingali ni mbegu ile ile, bali imeumbuka.

71 Sasa tunaona ya kwamba muumbuaji huyu amekuwa pia na muda kama huo wa wakati, wa kuumbua, kama Mungu alivyokuwa nao wa kugeuza. Sasa yeye aliipanda mbegu yake, ama, hakuipanda mbegu yake, alininii . . . katika bustani ya Edeni. Tangu wakati huo, amekuwa na miaka elfu sita ya kuiumbua Mbegu ya Mungu, Neno la Mungu; kuliumbua, kulifanya kitu tofauti; wakati yeye . . . mara ya kwanza ambayo Hawa alimsikiliza, na kujichukulia fungu moja tu dogo.

72 Kumbukeni, kwanza Shetani alilinukuu Andiko hilo vizuri tu vile lingaliweza kuwa, "Ati Mungu amesema ya kwamba, 'Msile kila mti katika bustani ya Edeni'?" Mnaona? "Msile kila mti?"

73 Na kumbukeni sasa, Hawa alisema, "Naam, tunaweza kula kila mti; ila mti ulio katikati ya bustani, haitupasi hata kuugusa." Sasa mwangalie, katika ujumbe wake, akiligeuza hilo Neno kidogo tu. Katika kusema . . . Hawa alisema, "Kwa

kuwa Mungu alisema, kwamba, kama tukifanya hivi, siku hiyo ‘tutakufa.’”

74 Akasema, “Loo, hakika hamtakufa.” Mnaona, yeye alikuwa ni mwa—mwanamume, akasema, “Wewe, fanya hili sasa. Na, wewe, kidogo ninyi ni watu wajinga. Nyinyi, kweli, hamjui mambo haya yote. Lakini kama tu ungeshiriki jambo hili, basi ungepata hekima, ungepata maarifa. Ungejua mema na mabaya na muwe kama miungu, ninyi, kama tu ungeshiriki hekima hii niliyo nayo. Ninajua, bali wewe hujui.”

75 Ambayo, ni vema kuwa na hekima. Bali kama hekima hiyo ni kinyume, kama hekima hiyo si hekima halisi kutoka kwa Mungu, hekima ya Kiungu, nayo inakuwa hekima ya kawaida; sijali tuna kiasi gani cha sayansi, na kadhalika, ama elimu, ni ya ibilisi. Nitawathibitishia, Bwana akipenda, katika dakika chache. Ni ya ibilisi.

76 Ustaarabu ni wa ibilisi. Ndio kwanza nimalize kuhubiri juu ya hilo. Utamaduni wote duniani, nguvu zote za sayansi, na kila kitu, ni cha ibilisi. Ndiyo injili yake aliyohubiri, ya maarifa, katika bustani ya Edeni. Naye amechukua maarifa hayo, maarifa yaliyopotoshwa, kinyume na Neno na mapenzi na mpango wa Mungu. Na sasa yeye amekuwa na miaka elfu sita kufanya vile Mungu alivyofanya hasa, ila tu katika njia iliyopotoshwa, naye akachukua muda ule ule wa wakati kuingiza Edeni yake. Sasa yeye ana Edeni hapa duniani, nayo imejaa hekima, maarifa. Hiyo ilikuwa ndiyo injili yake hapo mwanzo, maarifa, hekima, sayansi. Mungu kamwe hajawahi kushughulika na mambo kama hayo. Nami na—nataka mwangalie kwa dakika moja. Alifanya hili, na kwa sababu alikuwa ni mtu wa hekima ya kilimwengu.

77 Sasa, ni vigumu kusema jambo hili. Ni—ni vigumu sana, kwa sababu tukinena na watu wanaojisikia jinsi ninavyojisikia, na jinsi nimekuwa kwa muda wa miaka mingi. Lakini tangu kule kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba, juu ya hao Malaika nyuma tu ya ule mlima kule, *Hiki* kimekuwa ni Kitabu kipya. Ni mambo yaliyokuwa yamefichwa, yanafunuliwa kama vile Mungu alivyoahidi katika Ufunuo 10, angeyafunua. Nasi ndio watu waliobarikiwa ambao Mungu amewachagua, wa duniani, tuweze kuona na kuyaelewa mambo haya; ambayo si ya nia ya kisiri ya mtu wa kimwili akijaribu kuyabuni. Ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, likathibitishwa, kwamba ni kweli. Likathibitishwa, sio na sayansi; bali na Mungu, kwamba ni kweli. Mungu, kama nilivyosema hapo awali katika ujumbe, Mungu hahitaji mtu yeyote kulifasiri Neno Lake. Yeye Ndiye Anayejifasiria. Anasema litatukia, nalo linatukia. Hiyo ni, Yeye—Yeye hulithibitisha, hilo linalifasiri.

78 Miaka michache iliyopita wakati, sisi watu wa kipentekoste, wakati makanisa ha—hayo mengine yalipotwambia ya kwamba tulikuwa “wendawazimu,” wala “tusingeweza, Roho Mtakatifu

alikuwa ni kitu kilichopita." Bali tunaona ya kwamba ahadi ya Mungu ilikuwa ni kwa yeye atakaye, na sasa tunajua vinginevyo. Mnaona, na hiyo ni mambo haya kufunuliwa, kidogo kidogo tu.

79 Na sasa Yeye aliahidi ya kwamba siri zilizofichwa katika hizo, nyakati hizo zote za kanisa, zingefunuliwa moja kwa moja katika wakati wa mwisho. Naye anatujulisha sasa. Tuko katika wakati wa mwisho. Tuko hapa sasa.

80 Sasa, Shetani ndiye mwanzilishi wa ustaarabu. Yeye ni mwanzilishi wa sayansi. Yeye ni mwanzilishi wa elimu.

Mnasema, "Hiyo ni kweli?"

81 Vema, hebu tusome katika Neno la Mungu sasa, Mwanzo 4, na hebu turudi na tuone kwa dakika moja. Ninajua huenda mimi, kama nikichukua muda mrefu sana, Ndugu Carl labda ataniambia. [Mtu fulani anasema, "Ni sawa."—Mh.] Lakini, Mwanzo, mlango wa 4, na kifungu cha 16, inaendelea kusema hapa, hapo mwanzo, yale Mungu aliyofanya kusudi, apate kuweka laana juu ya mwanamume na mwanamke, na yote waliyopaswa kufanya; wala si *laana* juu yao, bali kuwaambia kile kingetukia, na kuilaani nchi kwa ajili ya Adamu. Nasi tunaona hapa sasa, ya kwamba Hawa alikuwa na mapacha. Na mmoja wao alikuwa ni wa Shetani, na mmoja wao alikuwa ni wa Mungu.

Sasa unasema, "Loo, la! La. Sasa, Ndugu Branham!"

82 Hebu kidogo. Hebu nitafutieni Andiko moja, mahali popote, ambalo linasema ya kwamba Kaini alikuwa ni mwana wa Adamu. Nitawaonyesha katika Maandiko ambapo yanasema, "Kaini alikuwa ni wa yule mwovu," sio Adamu.

83 Sasa angalia wakati alipochukua mimba hapa. Tutaanzia kwenye mlango wa 4, kwanza.

> *Adamu akamjua*. . .*mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, "Nimepata*. . . akasema sasa, *nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana.*

84 Hakika, ilibidi iwe. Haidhuru ilikuwa ni malaya ama yeyote yule, ilibidi aje kutoka kwa Mungu, mnaona, kwa kuwa hiyo ni mbegu Yake, ni kanuni ya mbegu Yake, itabidi izae hata kama ni mbegu iliyoharibiwa, iliyopotoshwa, ama chochote kile. Haina budi kuzaa, haidhuru. Ni amri Yake.

> *Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili.*

85 Hakumjua tena. Adamu alimjua mkewe, naye akamzaa Kaini na pia akamzaa Habili, mapacha. Shetani alikuwa pamoja naye asubuhi hiyo, Adamu alasiri hiyo.

86 Mmeona ule ubishi mkuu kwenye gazeti hapa, ninaamini, huko Tucson sasa, wa yule mwanamke akimzaa mtoto mweusi na mtoto mzungu, wakati ule ule. Yeye aliishi na mumewe asubuhi hiyo, na huyo mwanamume alasiri hiyo. Naye mwanamume huyo

angemtunza, huyo mzungu alisema angemtunza mtoto wake mwenyewe, bali huyu mtu mweusi ingempasa kumtunza wake. Mnaona? Ninajua hilo, katika kuwazalisha mbwa na kadhalika, hakika litatendeka, kama ni katika saa chache baadaye. Hili linalithibitisha.

87 Sasa kuonyesha mahali ustaarabu ulipotoka, sasa hebu na tusome Mwanzo hapa, katika mlango wa 4 wa Mwanzo tena, na tuone ni wapi. Kifungu cha 16.

> *Kaini akatoka mbele ya uso wa Mungu, akakaa katika nchi ya Nodi, mbele ya Edeni.*
>
> *Kaini akamjua mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Henoko; akajenga mji akauita Henoko, kwa. . .jina la mwanawe.*

88 Ustaarabu ukaanza. Daktari Scofield, hapa katika Biblia yangu ya Scofield, inasema, "Ustaarabu wa kwanza." Angalieni, ndipo akawazaa wana, nao wakatengeneza vinanda na muziki. Huyo mwingine aliwazaa wana, naye akaanza kufanya mambo mengine, maajabu, akajenga miji, na—na kutengeneza vyombo vya shaba, na vitu vya kila namna. Mnaona, hivyo ndivyo alivyofanya, ukawa ndio ustaarabu wa kwanza, ambao ulikuwa ni wa Kikaini. Amefanya jambo lile lile kote katika nyakati.

89 Sasa hebu tufike pale kwenye kifungu cha 25, tuone jinsi huo mwingine ulivyokuwa.

> *Adamu akamjua mke wake tena;* sasa, *akazaa mwana mwanamume, akamwita jina lake Sethi; maana alisema, Mungu ameniwekea uzao mwingine mahali pa Habili,* ambaye *Kaini alimwua.*
>
> *Naye Sethi. . .Sethi naye akazaa mwana, akamwita jina lake Enoshi.* Hapo *ndipo watu walipoanza kuliita Jina la Bwana* (kutoka upande wa Sethi, si upande wa Kaini).

90 Mnaona, ile elimu kuu ambayo sisi sote tunashikilia sana! Ukomunisti leo ni kitu gani, mungu wao ni nini? Ni elimu, sayansi. Tunafanya nini, haidhuru? Tunaishi wapi? Yatafakarini maneno haya leo.

91 Sasa ana aina yake ya Edeni, Shetani anayo sasa. Katika miaka hii elfu sita, yeye amefanya (sio kuumba), bali, kuumbua dunia nzima ya Mungu; viumbe vyake, wanyama, kuzalisha kwa kuchanganya mbegu, kuzalisha chotara; miti, mimea, binadamu; hata kufikia kwa dini, Biblia, kanisa; hata amejipatia bustani kamili ya Edeni, ya sayansi, kila kitu kikiendeshwa na sayansi. Motokaa zetu, kila kitu tulicho nacho, tulipewa na sayansi, yale mwanadamu aliyofanya. Naye anayo Edeni yake kuu hapa; kuthibitisha Ujumbe huu umekuja kwa wakati ufaao, kuthibitisha ya kwamba si wakati mwingine bali ni Ufunuo 10! Angalieni kule kuchanganya mbegu siku hizi, kufanya bora

zaidi, ama, ya kupendeza zaidi, sio bora. Waangalieni watoto wadogo leo hii.

92 Nilimpeleka binti yangu kwa daktari wa meno, jana, naye akasema meno yake yalikuwa yakienda kombo. Ndugu mmoja huko chini Tucson, Ndugu Norman, alikuwa na binti yake mdogo, nayo meno yake yalikuwa yakitokeza nje. Naye daktari wa meno anasema kwamba hivi karibuni, anaamini, ya kwamba labda katika nyakati zijazo, kwamba watu watazaliwa, meno yakimea vyovyote. Ni chakula tunachokula, chakula chotara.

93 Hivi mlisoma Reader's Digest, mwezi uliopita, kuhusu Billy Graham, yule mwinjilisti muungwana? Mmekuwa mkimsikiliza? Ninamwombea sasa kuliko hapo awali. Wakati alipozungumza na wale wenye ukosi uliopinduliwa, na kadhalika, hivi majuzi usiku, akiwakemea makasisi. Jambo fulani limempata. Moja ya siku hizi, ninatumaini ataona mahali alipo, angalieni, sasa anaita kutoka Sodoma, ule mji uliopotoka. Na sasa angalieni hii kwenye Reader's Digest, Billy alikuwa amedhoofika sana hata asingeweza kuiendeleza mikutano yake. Nao wakamwambia ilimbidi kukimbia, kufanya mazoezi, na kadhalika. Kwa hiyo yeye hukimbia maili moja kwa siku, naamini ndivyo, ama kitu fulani, kupata mazoezi.

94 Mwanadamu ameoza. Jamii yote ya binadamu imepotoka. Kila kitu ni kama ilivyokuwa katika wakati uliotangulia ile gharika. Yote yamevurugika kabisa, yakageuzwa, tofauti na safu iliyonyoka ambayo Mungu aliwapanda. Dhambi, kupitia kwa sayansi na udanganyifu, imeivuruga jamii nzima ya binadamu.

95 Mlisoma pia chini ya makala hiyo, ambapo ilisema, "Siku hizi, ya kwamba wasichana wadogo na wavulana wako kwenye umri wao wa makamu, kulingana na maumbile ya kimwili, kati ya umri wa miaka ishirini na ishirini na mitano." Wazieni hilo.

96 Katika utambuzi hivi majuzi usiku, nilimpata msichana mwenye umri wa miaka ishirini na miwili, katika kukoma hedhi, nikamwita. Na hivyo ndivyo daktari wake alikuwa amemwambia.

97 Mnaona, ni jamii iliyoanguka, potovu, inayoelekea kuzimu. Ninajua hilo linasikika lisilo na maadili, bali ni la Kibiblia, mnaona, kwamba ni kweli; na jamii hii tunayoishi, kizazi hiki cha watu.

98 Sasa angalieni siku hizi, kuzalisha ng'ombe kwa kuchanganya damu, kuzalisha mimea kwa kuchanganya mbegu; nayo sayansi inarudi moja kwa moja huku, sayansi ile ile inayofanya hilo, inasema, "Hicho ndicho kinachoangamiza jamii nzima ya binadamu." Mnayasoma jinsi ninavyoyasoma. Vema, kwa nini hawaikomeshi? Ni kwa sababu hawawezi kuikomesha. Neno la Mungu limesema ingekuwa jinsi hiyo. Lakini kama wangewazia kwa dakika moja, wao ni vyombo, kama vile Yuda

Iskarioti, likitimiza hasa kitu kile ambacho Mungu alisema kitatukia. Linatukia tu kabisa kwenye msingi wao wa sayansi.

99 Kwa utafiti wake wa kisayansi, katika mpangilio ule ule alimdanganya Hawa, amelidanganya kanisa pia, ambapo Hawa pale alikuwa ni mfano. Sasa, sasa Adamu ni mfano pale tena, ama Hawa, hasa, wa kanisa, angalia kile alichofanya. Kupitia kwa kutangatanga kwa ajili ya maarifa, anavuka mpaka kati ya mema na mabaya, kwa kusikiliza upotovu wa Shetani, ama uumbuaji, wa Neno asili la Mungu.

100 Na sasa makanisa leo yameumbuka. Sasa sizungumzi juu ya watu, watu binafsi. Ninazungumza juu ya ulimwengu wa kanisa. Moja limeumbuliwa kwa njia moja, lingine limeumbuliwa vingine, na, kwa sayansi. Mpangilio ule ule aliofuata. Yeye ametekeleza tishio lake, Shetani amelitekeleza, la Isaya 14:12.

101 Hebu tusome tu hilo kwa muda kidogo. Katika Kitabu cha Isaya, hebu tuanzie mlango wa 14, kifungu cha 12.

> *Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe Lusifa, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyeyaangusha mataifa!*

Huyu ni Isaya akimwona katika ono, mnaona, katika wakati ujao.

> *Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, . . . pande za mwisho za kaskazini.*

102 Kusudi la Shetani, kutoka Edeni, lilikuwa ni kujifanyia Edeni yake mwenyewe; na kujiinua juu, ili kwamba nyota za Mungu zimwabudu, wana wangemwabudu. Na amelitekeleza kabisa sasa, na wakati amefanya jambo hili na kuliingiza kanisani. Ambalo, sitaingia katika utondoti. Yeyote wenu anayezisikiliza kanda hizo anajua hilo. Ya kwamba, hiyo ndiyo saa tunayoishi hasa, na Shetani ndiye amefanya jambo hilo kupitia kwa miradi ya elimu, pambo bora, *hiki* kilicho bora zaidi, na *kile* kilicho bora zaidi. Na bila kujua, wakati wote, wanaenda moja kwa moja kuelekea mautini. Vipofu, wakiwaongoza vipofu wenzao, viongozi wa mataifa waliopofushwa, viongozi wa sayansi waliopofushwa, viongozi wa kanisa waliopofushwa, vipofu wakiwaongoza vipofu wenzao. Yesu alisema, "Waacheni, wote wawili wataanguka shimoni."

103 Hapa angalieni mfano wa Edeni hizi mbili zikifananishwa kwa karibu sana, mpaka karibu ziwadanganye walio Wateule. Mathayo 24:24 ilisema ya kwamba ingekuwa hivyo. Lakini ninataka kusimama kwa dakika chache na kuzitafakari Edeni hizi mbili, na jambo moja hasa, jinsi ambavyo Biblia inatwambia ya kwamba Neno la Mungu kweli liliitoa Edeni hiyo, na jinsi ambavyo Neno la Mungu linavyotuonya ya kwamba Edeni hiyo nyingine ingekuja.

104 Sasa, pia tunajua ya kwamba hapana budi kuweko na Edeni nyingine, kama tungemsikiliza nabii pia, Paulo, katika Wathesalonike wa Pili mlango wa 2. Ningeweza kupasoma mkitaka.

> Yeye ajiinuaye nafsi yake*; siku* hiyo *haiji,* ya Bwana, hata *akafunuliwa yule mtu wa kuasi,* . . .
>
> . . .yeye aketiye katika hekalu la Mungu, akijiinua *nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu,* hata yeye kama Mungu kuabudiwa kama Mungu.

105 Wazia juu ya hilo! Sasa Isaya 14, nabii alisema ya kwamba alimwona "Lusifa, moyoni mwake," kwa ono chini ya uvuvio wa Mungu, "akisema angefanya hivyo." Katika Isaya, miaka mia nane kabla ya Paulo, ama karibu hiyo.

106 Sasa hapa, miaka mia nane baadaye, Paulo anamwona, akija mahali pake. Angalia, inaishia, kwenye Edeni yake; Edeni yake ya kisayansi, pamoja na ulimwengu wake wa kisayansi, pamoja na kanisa bibi-arusi wa kisayansi, yote chini ya ne—neno la "maarifa," seminari kuu, digrii kuu, utaratibu wa elimu.

107 Sikilizeni, ndugu, dada, kila mmoja wetu atapitia kwenye barabara hiyo ambayo Florence aliipitia. Ninawauliza, katika Jina la Yesu, kutafakari Hili. Sio kunitafakari mimi. Mimi ni ndugu yenu. Hilo, hilo silo. Tafakarini Neno ninalosema, la Biblia ya Mungu. Na muangalie, limethibitishwa kikamilifu katika Neno la Mungu Mwenyewe, katika wakati tunaoishi, mahali tulipo sisi.

108 Utaratibu huu wote ni upinga Kristo mtupu, wenyewe. Sasa, hana budi kuwa na Edeni, alisema atakuwa nayo. Hili hapa Neno rahisi la Mungu likisema ya kwamba angefanya hivyo, na hapa tunaangalia moja kwa moja huko na kumwona akilifanya. Amelifanya kwa bibi-arusi wake wa kimadhehebu, kielimu, kisayansi. Yeye atachukua uongozi, moja ya siku hizi, katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni ambalo litaanzishwa. Wote watakuwa pamoja naye. Kujaribu . . .

109 Hao watu, sio kwa sababu ni watu wabaya; walipandwa kwenye safu hiyo iliyonyoka, kama mahindi, bali Shetani akapanda vile vitambaazi, vinavyoitwa sayansi, utafiti, elimu, digrii za udaktari. Wakati mwingine hata hawatakuruhusu mimbarani isipokuwa iwe unaweza kuonyesha digrii ya udaktari kutoka kwenye seminari mahali fulani. Yote ni makosa! Sio hao watu; utaratibu ndio mbaya. Na sasa limefanya nini? Lote linaelekea tena, na kuleta ulimwengu wote mzima (kwa lundo la kuchanganya mbegu, kuipotosha Mbegu asilia ya Mungu) kwenye giza lingine la mchafuko.

110 Lakini ninashukuru sana kwamba Mungu anatujali tena, ya kwamba angali anaweza kutenda kazi juu ya hali za mambo. Aliahidi angefanya hivyo, na kuita kundi dogo ambalo lingekuwa ni Bibi-arusi Wake.

111 Angalieni hapa tena sasa, jinsi ambavyo makanisa haya yanawakilisha kikamilifu, ama Edeni hizi.

112 Mungu, kwa Mbegu ya Neno Lake! Na kuna kitu kimoja tu kinachoweza kulihuisha Neno, na hicho ni Roho, kwa kuwa Ndiye Mtoa-Uzima kwa hilo Neno. Na hapo Uzima ulio kwenye Neno unapokutana na Uzima wa Roho, unazaa chochote Mbegu hiyo ilicho.

113 Sasa angalieni kile kilichotukia. Katika bustani ya Edeni kulikuwako na uchumi wa Mungu wa kutokuwa na hatia, na huo ulikuwa ni mmoja wa vi—vipindi vya wakati. Kipindi cha kwanza cha wakati kilikuwa ni kutokuwa na hatia, hao watu hawakujua dhambi. Hawakujua chochote kuhusu dhambi. Adamu na Hawa wote wawili walikuwa uchi, bali walifichwa uchi wao, kwa pazia la roho usoni mwao. Kamwe hawakujua kwamba walikuwa uchi, hata kidogo, kwa kuwa walifichwa. Kwa maana, pazia la Mungu juu ya nia zao wenyewe, hawakujua mema na mabaya yalikuwa ni nini. Nao hao wote wawili wakisimama pale uchi, ilionyesha ya kwamba ujuzi huo haukuwa umewafikia, mnaona, kwamba walikuwa uchi. Hao wawili walikuwa uchi wala hawakujua.

114 Sasa kama mtafungua, mkitaka, ama kuandika, Ufunuo, mlango wa 3. Roho Mtakatifu akiutabiri wakati huu wa mwisho, kwa Wakati wa Laodikia wa Kanisa la Kipentekoste katika siku za mwisho, Yeye alisema, "Nawe ni uchi, na ni kipofu, wala hujui."

115 Hiyo hapo Mbegu ya Mungu, chini ya kutokuwa na hatia, pasipo kujua kabisa walikuwa uchi, chini ya pazia la Roho Mtakatifu, akiwafunika kutokana na dhambi.

116 Na sasa katika wakati wa mwisho wa kanisa, tunaona hapa ya kwamba wao ni uchi tena, wala hawajui. Lakini si pazia la Roho Mtakatifu. Ni pazia ambalo Shetani alimfunika kisiri Hawa huko nyuma, pazia la tamaa mbaya, pazia la tamaa mbaya. Hao ni wachafu sana hata hawajui kwamba wako uchi, wanawake wetu mitaani, wamevaa kaptura, nguo za kizinifu.

117 Mtu fulani alinitumia kipande cha gazeti hivi majuzi, cha hii nguo mpya ambayo watavaa, nafikiri, inchi kumi na nne kutoka nyongani, ama kitu kama hicho. Nami nashangaa kama nanii wetu—kama wanawake wetu wanatambua ya kwamba hilo ni pazia la tamaa mbaya?

118 Sasa u—ungesema, "Ninaweza kuthibitisha, mbele za Mungu, ya kwamba sina hatia ya uzinzi wowote kwa mume wangu, ama ni—ni . . . yote haya."

119 Lakini hata hivyo, kwenye ile Hukumu, utaitwa "mzinzi." Biblia ilisema hivyo. Yesu alisema, "Kila amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani, amezini naye tayari moyoni mwake."

120 "Vipofu, uchi, wala hawajui!" Si maskini wanawake hao huko nje; sina kitu dhidi yao. Ni ule uovu! Na mfumo wa kanisa unaonekana kushindwa kuutambua ama kuupinga; unawaacha wakate nywele zao, wajipodoe, na kaptura na kadhalika, chini ya jina la Ukristo. Ni jambo la kuchukiza jinsi gani! Mnaona, wao ni uchi tena, katika Edeni ya Shetani, wala hawajui. Hawajui hilo.

121 Ninaamini ninaona, labda, nikiangalia hapa, kidimbwi cha kuogelea, ambacho wanawake huko nje sasa. Laiti yule mwanamke angetambua kile anachofanya, bali hajui. Yeye yu uchi. Mwili wake ni mtakatifu. Anavua nguo ambazo Mungu alimvisha, kwa ngozi, kwa ajili ya kizazi hiki. Yeye daima anaikatilia mbali. Yu uchi, chini ya neno la "ustaarabu, elimu ya juu, ustaarabu bora zaidi, maadili ya juu zaidi." Hebu nihakikishe ya kwamba hili linazama ndani. Yote ni ya ibilisi, na yataangamizwa katika Kuja kwa Bwana Yesu. Yataangamizwa, kila chembe. Hakutakuwako na kitu kimoja kilichosalia.

122 Na, loo, rafiki, kote nchini, wakati mkinisikiliza hapa Phoenix, wazieni mambo hayo! Mko hapa mkiyategemea. Sasa, Yesu alisema kwamba, "Yangewapoteza walio Wateule kama yamkini."

123 Roho wa kwanza alikuwa ninii...pazia la kwanza lilikuwa ni pazia takatifu, Roho Mtakatifu, naye hakupaswa kuangalia nje ya Hilo. Lakini wakati—wakati Shetani alipoanza kuzungumza naye kuhusu maarifa, ilimbidi tu kuuchungulia ulimwengu kidogo.

124 Na hivyo ndivyo hasa binti yake, kanisa, limefanya. Inakubidi kuona, inakubidi kuvaa kama mchezaji wa sinema, ama vijana wa kiume inawabidi kutenda kama Elvis Presley ama—ama Pat Boone, ama—ama baadhi ya watu hao, chini ya jina la dini.

125 Pat Boone ni wa Church of Christ. Elvis Presley ni Mpentekoste. Watu wawili waliopagawa na pepo ambao wameutupilia ulimwengu kwenye machafuko mabaya kuliko Yuda Iskariote alivyofanya katika kumsaliti Yesu Kristo. Hawajui hilo. Hao wavulana hawajui hilo. Sina neno dhidi ya hao—hao wavulana, wanaume, ni roho ambayo inachochea hayo.

126 Hebu sogea kidogo tu upande mmoja, hebu kitambaazi hicho kishike tu shina la mhindi huo, wakati mmoja, angalia kitakachotukia; huo mhindi umekwisha. Loo, naam, tayari kimeupata. Na hivyo ndivyo kitakavyofanya. Kitafanya hivyo kila wakati. Ilimbidi Hawa kuutupia ulimwengu jicho moja tu.

127 Na hebu niwaambie jambo fulani, ndugu na dada. Katika Yohana wa Kwanza, mlango wa pili na kifungu cha 15, tunaweza kukisoma mkitaka, Biblia inasema:

> ...*Tukiipenda dunia,* au mambo yaliyomo katika dunia, ni kwa sababu *kumpenda* Mungu hata *hakumo ndani* yetu.

128 Sasa, neno hapo si *dunia*; ni neno la Kiyunani, ni *kosmos*, ambalo linamaanisha "utaratibu wa ulimwengu." Kama tukiipenda mitindo ya dunia, ulimwengu, kama tukiupenda mwelekeo wa kisasa, kama tukifikiri "huu ni wakati mzuri sana, loo, tunayo mambo haya yote," kama ukiwazia hayo, ni kwa sababu mawazo yako ni mabaya. Yamepotoshwa na ibilisi. "Kwa maana ukiupenda utaratibu wa dunia, na mambo ya ulimwengu huu wa sasa, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Kumbukeni hilo. Ee Mungu! Angalia kile tunachoangalia!

129 Hapa nataka kusimama kidogo tu na kuwaambia hadithi ndogo. Nilimsikia kasisi wa jeshi kutoka kwenye Vita Vya Kwanza vya Dunia. Walikuwa wametupa . . .

130 Kama vile Shetani hapo mwanzo, wakati alipoingia katika bustani ya Edeni. Asingeweza kuzichimbua Mbegu hizo. Asingeweza kuziangamiza. Bali alizinyunyizia sumu, na kuiumbua Mbegu, haikuzaa kwa jinsi yake. Iliumbua Mbegu ya asili.

131 Na hivyo ndivyo taratibu hizi zote za dini. Wangali ni wana na binti za Mungu, bali wanaumbuliwa. Wanaenda kanisani, wakitaka kufanya mema. Mtawa wa kike haingii kwenye nyumba ya watawa apate kuwa mwanamke katili. Mhudumu kamwe hapitii shuleni apate tu kuwa mtu m—m—mbaya. Kamwe hujiungi na kanisa, na kupeana mikono, ukaandika jina lako kwenye kitabu, ama lolote ufanyalo kanisani mwako, upate kuwa mtu mbaya. Unafanya hivyo kuwa mtu mzuri. Bali ni ule udanganyifu, ni ule uumbuaji unaofanya jambo hilo. Shetani aliinyunyizia. Mnaona? Mungu kamwe hakuwa na dhehebu. Hakuna kitu kama hicho kinachopatikana mahali popote katika Maneno ya Mungu.

132 Mungu ndiye dhehebu letu, tumeshirikishwa katika Yeye, Mwili, katika Mungu, Mbinguni. Hiyo ni kweli. Majina yetu yamo kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Angalieni.

133 Lakini, mnaona, ninajua ni vigumu sana, lakini na—nawatakeni mvumilie tu muda kidogo zaidi mkiweza. Katika wakati wa vita vya ulimwengu . . . Samahani kwa kuondoka kwenye somo langu.

134 Lakini ili kujenga hoja hii, ni—ninataka kuwapa uchanganuzi wangu wa yale Shetani aliyofanya huko Edeni: alinyunyizia sumu kali mno. Mngetaka kujua kinyunyizio hicho kilikuwa ni nini? Ninaweza kuwaambia. Nina fomula yake, maneno mawili: kutokuamini, ambako ni kinyume cha imani, alinyunyizia kutokuamini, shaka. Ndipo sayansi ikapajaza mahali pake. Mahali palipo na pengo, lililoingia kwenye Mbegu, Shetani alilijaza pengo hilo kwa maarifa na sayansi na ustaarabu, nayo imeumbua wote, uumbaji mzima wa Mungu.

135 Najua mnafikiri ninawasukumia kwenye tawi, bali niko kwenye tawi pamoja nanyi. Nasi sote tupo hapa tukijaribu kuona kile tunachoweza kufanya. Hatuyasemi mambo hayo tupate kuwa tofauti. Hatuna budi kuwa waaminifu.

136 Sisi, kila mmoja, anafikia kwenye mwisho wa safari, ambako tutatoa hesabu kwa ajili ya kila neno. Sasa hivi, tunajua ya kwamba sauti zetu. . .Tunapozaliwa, kilio chetu kidogo cha kwanza chote huingia kwenye kanda. Itachezwa tena kwenye Siku ya Hukumu. Hata nguo unazovaa zitaonyeshwa usoni pako, kwenye Siku ya Hukumu. Hata sayansi imepata kujua jambo hilo, kwa televisheni. Mnaona, televisheni haitengenezi picha, inaipitisha tu. Rangi za nguo, kila unaposogea, kila wazo niani mwako, linawekwa kabisa kwenye kumbukumbu ya Mungu. Na kitu hicho kikubwa kitawekwa moja kwa moja mbele zako, kila moja ya hizo nguo chafu ulizovaa; kila wakati ulipoingia kwenye duka la kinyozi, ukazikata hizo nywele ambazo Mungu alikupa. Itakuwa. Utaliwajibikia. Huwezi kusogea papo hapo, hata mawazo ya moyo wako wakati ukifanya hilo, yatachezwa papo hapo mbele zako. Utaponaje? "Tutapataje kupona tusipoujali wokovu mkuu namna hii?" Mnaona? Hatutapona. Kila msogeo, na mawazo ya moyo, yanarekodiwa moja kwa moja katika kiwango kingine, hata rangi za nguo mnazovaa. Televisheni, televisheni ya rangi inalithibitisha moja kwa moja, inalivuta na kulionyesha, mnaona, na hicho ni kiwango kimoja tu kutoka kwa vile vitatu tunamoishi. Mnaona?

137 Sasa jinsi ambavyo sumu imelipiga kanisa, imeipiga dunia! Sumu ya Shetani juu ya hizo Mbegu, imetia mapengo ndani yake na kuifanya iumbuke. Zaidi na zaidi, yeye huingia ndani ya mioyo ya makanisa, na katika mioyo ya watu na kila kitu, sayansi, sayansi. Mpaka imekuwa mahali ambapo jamii ya binadamu, kwa kuchanganya damu. . .Ninaamini kila mbegu inapaswa kuzaa kwa jinsi yake. Na jamii ya binadamu, na mmea, na yote kwa kuchanganya mbegu, imetufikisha mahali; katika kula chakula chetu kutoka ardhini, ambacho, miili yetu, imefanywa chotara, imeingiza bongo zetu zote. . .Sasa, kama miili yetu inashuka, kutoka kwenye umri wa miaka ishirini hadi ishirini na mitano, kwa sababu ya seli zilizoharibika, kwa chakula chotara, je! seli zetu za ubongo haziharibiki? Je! hizo si ni seli, pia? Hiyo ndiyo sababu Ricky anaenda kasi hapa barabarani, kwa gari la mbio mno; wakati Ricketta, Elvitta, na wengi wao, kama tunavyoweza kuwabandika jina, yuko huku nje nusu uchi mbele za watu, ameingia wazimu kabisa, hana tena dhana ya heshima ama uadilifu.

138 Tuiendee hadithi yangu ndogo. Kasisi huyu wa jeshi alisema alikuwa huko chini hospitalini, na akasema wavulana wengi sana wamelazwa hemani, baadhi. . .Alikuwa tu ndio ametoka huko nje. Alisema alienda huko nje, ndipo afisa fulani akamwambia, kasema, "Kasisi, tunataka kwenda huko nje,

tuziangalie zile mbuga huko nje." Walikuwa wamerusha sumu hii ya mvuke na ya gesi ya klorini, jinsi walivyofanya katika siku hizo.

139 Kisha kasema, "Nilitoka nikaenda huko nje, Ndugu Branham," kasema, "hapakuwapo na gome kwenye mti, hapakuwapo hata na unyasi. Ilikuwa kwenye asubuhi ya Pasaka." Akasema, "Kulikuwako na mabaki ya maskini vifaru vilivyoharibikia huko chini, ilibidi huyo afisa aandike kumbukumbu zake, aone kama yangeweza kufanyiwa jambo lolote, karibu na Msitu mnene wa Argonne." Kasema, "Nilipokuwa nimesimama pale peke yangu," kasema, "niliangalia juu, kasema, 'Ee Mungu, hivi ndivyo yote yanaishia.'" Hiyo ni kweli, yote yanakuja. Vyote vilikuwa vimeteketezwa, hapana uhai popote kamwe, nyasi zimeteketezwa; mti, na gesi hizo, miti ikauawa, kila kitu kikauawa, kikakunjamana, kimening'inia chini, ambapo kilishambuliwa kwa risasi na kadhalika.

140 Kama hiyo si picha ya ulimwengu leo, ambamo Shetani ananyunyizia kutokuamini kwake, uchotara wake, sayansi yake, maarifa yake! Mpaka, kile kilichokuwako hapo mwanzo, wakati Mungu alipomweka Adamu na Hawa katika ile bustani, ile paradiso nzuri isiyo na mauti, isiyo na maradhi, isiyo ya huzuni, na kila kitu ni kikamilifu na katika utaratibu, angalia vile DDT ya Shetani imefanya! Imo katika mchafuko. Hakuna kitu kilichosalia ndani yake.

141 Akasema, "Nikaanza kulia. Nikarudi nyuma, nilivutiwa kwenye mwamba fulani." Kasema, "Nilienda tu pale na kuuangalia huo mwamba, nikauvingirisha. Hapo chini ya mwamba huo kulikuwako na ua dogo jeupe likikua, kitu pekee kilicho hai kilichosalia, kwa kuwa lilikuwa limekingwa na mwamba."

142 Mungu, Mwamba wangu, tukinge leo, Ee Mungu, wakati sumu hizi zinapopepea kila mahali kwa jina la sayansi na elimu. Tukinge. Niweke hata siku hiyo, Ee Mungu, ndilo ombi langu. [Mtu fulani jukwaani anasema, "Usijipimie wakati wowote, Ndugu Branham."—Mh.] Sasa natumaini ya kwamba sisi, kila mmoja, tuko chini ya Mwamba huo, Kristo.

143 Ndio kwanza nihubiri hivi majuzi, wengi wenu mliusikia. Nilikuwa nikishuka kupitia mwituni, nikiwinda, nami nilijisikia kugeuka. Ndipo nikaangalia, na hapo palikuwapo na katoni ama pakiti tupu ya sigara, ama chochote mnachookiita. Na ni kampuni, sijisikii kulitaja jina lao, bali kampuni hiyo ya tumbaku ilikuwa, walikuwa na wito, "Chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mvuta sigara."

144 Nikaanza kutelemka ki—kidogo mwituni, na kitu Fulani kikanivutia, "Rudi kwenye pakiti hiyo ya sigara."

145 Nikawazia, "Baba wa Mbinguni, ninashuka kwenda hapa chini kwenye ule mti ambapo wale kuchakulo walinenwa na Wewe wakawa, asubuhi moja. Kwa nini uniite nirudi?"

146 Ndipo kitu Fulani kikasema, "Una mahubiri yanayokuja kwa ajili ya Jumapili. Somo lako limeandikwa juu yake."

Nikawazia, "Juu ya pakiti ya sigara?" Nikarudi.

147 Ndipo nikaanza kuwazia, "Chujio la mtu mwenye busara," ni udanganyifu wa jinsi gani huo! Kama mtu alikuwa na busara, asingevuta sigara kamwe. Lakini, mnaona, watu wanameza hayo.

148 Ninaamini ilikuwa ni miaka miwili iliyopita, wakati nilipokuwa kwenye moja ya ile mikutano, nikapanda nikaenda kwenye maonyesho ya dunia wakati yalipokuwa kwenye Pwani ya Magharibi. Nao walikuwa na picha ya Yul Brynner na wengi wao pale. Nao wanasayansi, wengi wao, walikuwa kwenye ukumbi ule ule, juu ya madhara ya kuvuta sigara. Jinsi ambavyo walipitisha moshi huo kwenye marumaru, kisha wakachukua ncha-Q ndogo na kuchota nikotini kutoka mle na kuiweka kwenye mgongo wa panya, kisha wakamweka kizimbani, katika siku saba alikuwa amejaa kansa sana hata asingeweza kutembea. Mnaona? Akasema . . . Akaipitisha kwenye maji.

Kasema, "Ati chujio!"

149 Kasema, "Ati chujio? Hakuna kitu kama hicho." Kasema, "Ukininii . . . " Sasa, hawa ni wanasayansi wenyewe. Wakasema, "Huwezi kuwa na moshi isipokuwa uwe na lami. Lami ndiyo inayotoa moshi."

150 Na jambo pekee ni kwamba, ni kiinimacho, wapate kuuza sigara nyingi zaidi. Wakati hiyo, kama nikininii . . . Situmaini mnafikiri mimi ninakufuru ama ni mlokole. Huyo ni pepo ndani ya mwanadamu, anayemfanya avute sigara, apate kujiua. Wakati a—anapohitaji nikotini ya sigara moja, ambayo itaridhisha tamaa yake, sasa kampuni inajitokeza na kiinimacho hiki cha udanganyifu, na kusema, "Chujio la mtu mwenye busara." Itambidi kuvuta sigara nne ama tano, kupata lami ya kutosha ndani yako (kumridhisha) kama uliyopata kwa sigara moja. Wamarekani wakiwauzia ndugu na dada zao mauti! Silielewi.

151 Lakini hata hivyo mle ndani, niliwazia, "Lipo Chujio la mtu mwenye busara ambalo ni la kweli."

152 Sasa kama mtu alikuwa akivuta sigara, kumbukeni, inatoa ladha ya mvuta sigara. Halafu, kama huwezi kupata ninii . . . kuridhisha tamaa ya kuvuta sigara mpaka utakapopata moshi pale na upate . . . haina budi kutoa ladha. Kwa hiyo unavuta sigara nne, ama tano, na zinakugharimu zaidi ya vile ungelipia kama ungalivuta tu sigara moja ya kawaida. Unaona, ni kiinimacho, kiinimacho cha uchuuzi; kuwadanganya

watu, Wamarekani. Ninapowazia juu ya Bonde la Forge, George Washington; huku theluthi mbili za askari wake, na hawana viatu miguuni mwao, kwenye siku hiyo ya baridi, wapate kututengenezea uchumi tulio nao! Halafu Wamarekani wanamwuzia Mmarekani, ndugu na dada yake, mauti, chini ya kiinimacho cha uongo, kwa fedha ya aibu, shina la mabaya yote. Tamaa kuu, kupenda fedha. Kitu hicho chote kimeingia wazimu, bila kujua ya kwamba kitu hiki chote kitaangamia! Lakini usipopata moshi, huwezi kupata ladha.

153 Ndipo nikawazia, "Lipo Chujio la mtu mwenye busara." Chujio la mtu mwenye busara! Ndipo nikachukua somo langu kutoka kwa "Chujio la mtu mwenye busara hutoa ladha ya mtu mtakatifu."

154 Kwa hiyo niliwazia kwamba madhehebu yetu yamefanya mambo mengi sana kama hayo, kuwachukua watu na kujiita Wakristo ambao wako tu vivi hivi. Kwa nini? Wanawapata wengi kwenye madhehebu ama mashirika yao. Tunawapata wengi mle ndani kwa kuwa tunawaacha waingie chini ya *hili*, *lile*, na hilo *lingine*, na chochote kile. "Hilo halileti tofauti yoyote, mradi tu wanaweka jina lao kwenye kitabu na kusema wao ni Wakristo. Hivyo tu. Loo, 'kwa imani unaokolewa.' Inakubidi kuamini." Ibilisi hufanya jambo lile lile. Naam.

155 Huna budi kuzaliwa mara ya pili, na huko huja kwa Chujio la Mungu! Sasa kuna Chujio la mtu mwenye busara. Nimelishikilia mkononi mwangu. Halitaleta ladha ya kimadhehebu, bali hakika litaridhisha ladha ya mtu mtakatifu, mwajua.

156 Mwanamke aliyekata nywele zake angepitiaje kamwe kwenye Chujio hili? Mwanamke aliyevaa kaptura angewezaje kupitia Humo, ama suruali fupi, wakati Biblia inasema, "Ni chukizo kwa Mungu, kwa mwanamke kuvaa mavazi ambayo hata yanampasa mwanamume"? Na mwanamume anayejiwazia lolote, anawezaje kutoka hapa nje na kuvaa kama wanawake, kuachilia nywele zake zikue kama za mwanamke, kufikia machoni mwake, pamoja na vichega nywele, na zimesokotwa namna *hiyo*? Yeye anavaa nguo za ndani za mkewe. Mke anavaa nguo za nje za mumewe. Ati chujio la mtu mwenye busara? Mtu mwenye busara hatafanya hivyo, wala mwanamke mwenye busara hatafanya hivyo. Neno la Mungu halitaliacha lipite.

157 Hakuna kitu kimoja kingaliweza kupitia kwenye Neno hilo. Hilo ni Roho Mtakatifu, Naye huliingiza Neno ndani yako, na Hilo hutoa ladha ya mtu mtakatifu.

158 Angalieni leo hii, Ricketta mtaani, umbo la kupendeza, rembo alilopewa na Mungu, naye Shetani analitumia. Naye atavalia kizinifu sana, bila kujua ya kwamba juma moja tangu sasa huenda atakuwa anaozea kaburini.

159 Nikishuka kuja mtaani hapa sio muda mrefu uliopita. Nilikuwa nikihubiri mkutanoni katika Assemblies of God

kwenye Pwani ya Magharibi, katika mkutano huko kwenye Shule ya Biblia ya Kusini-magharibi. Maskini msichana mdogo akitembea barabarani, maskini . . . amevaa hizo nguo ndogo, bikini, chochote unavyoziita, na matamvua yananing'inia chini, amevaa kofia na buti za kaoboi. Nilikuwa nikipanda kwenda barabarani. Nikawazia, "Maskini jamaa huyu, mtoto wa mama na baba fulani, aliwekwa hapa apate kuwa binti ya Mungu, naye amekuwa chambo cha mtego wa ibilisi." Nikawazia, "Ninaamini nitageuka tu nirudi, na kumwambia mtoto huyo." Alionekana kuwa ni rika la Sara wangu pale, umri wa miaka kumi na saba, kumi na sita, ama kitu kama hicho. Nikawazia, "La, afadhali nisirudi. Nitapanda tu hapa juu barabarani nikamwombee. Kama mtu fulani aliniona nikisimama na kuzungumza naye, afadhali nisifanye hivyo."

160 Sasa, pia sikilizeni, enyi wana wa Mungu, mnafikia mahali papo hapo, Mayezebeli hawa wa kisasa wanajipendekeza kwenu, bali mtu mwenye busara atawazia kwanza. Huenda akawa ni mrembo sana, huenda "nitapendeza sana nikiwa naye," bali hiyo itakugharimu nafsi yako, ewe mvulana; baadhi yenu wasichana, kwa hawa akina Ricky! Chujio la mtu mwenye busara hutoa ladha ya mtu mtakatifu.

161 Ninyi wanaume mliooa, mnapowaona hao wanawake mtaani namna hiyo, ninyi wana wa Mungu, hivi hamtambui kile kilichotukia hapo mwanzo? Wakati sayansi ilikuwa imewafanya wanawake warembo sana katika siku zilizoutangulia ulimwengu wa ile gharika, mpaka wana wa Mungu wakawachukua binti za wanadamu (sio binti za Mungu), na Mungu kamwe hakusahau hilo. Waliangamiza kitu hicho chote; sayansi, warembo zaidi. Ilikuwa kwamba . . . Mnaona urembo wa wanawake ukiongezeka katika siku za mwisho, ni ishara ya wakati wa mwisho; Mungu amethibitisha hilo. Kwa hiyo, tumia Chujio la mtu mwenye busara, utakuwa na ladha ya mtu mtakatifu. Itakugharimu nyumba yako. Itakugharimu wadhifa wako. Itakugharimu kila kitu ulicho nacho; mbali na hayo, nafsi yako! Itaivunja nyumba yako. Huenda ikamfanya mwanamume mwingine kuwalea watoto wako, ama mwanamke mwingine kuwalea watoto wako.

162 Chukua Chujio la mtu mwenye busara, litatoa ladha ya mwanamke mtakatifu. Unapoanza kwenda kwa kinyozi, ama kitu kama hicho, nao wanakwambia, "Utaumwa na kichwa, wajua." Chukua Chujio la mwanamke mwenye busara, yale Biblia iliyosema, unaona, kisha uyaondokee. Unaona? Usifanye hivyo.

163 Mimi ni ndugu yenu, nami nawapenda. Sina kitu dhidi yenu. Mungu anajua. Na hilo ndilo linalonifanya niseme mambo nisemayo, ni kwa sababu ya—ya mapenzi ya Mungu kwenu. Kama mtu angetoka aende huko nao wasikwambie, mchungaji wako akuache uketi huku na kufanya jinsi hiyo, yeye hakupendi. Hawezi kukupenda. Nisingetaka upendo wa namna hiyo kwa

wanawake. Ninataka kuwa na ladha takatifu kwa dada yangu. Ninamtaka kweli awe ni dada yangu. Sio mtu anayeweza kusema, mtu kuzungumza juu yake kuwa mrembo sana na jinsi alivyo, na hao malkia wa jinsia, "Yeye anaenda kwa ninii yangu . . . " A-ha. La. Ninamtaka awe bibi wa heshima!

164 Ee Bwana, nidumishe chini ya Mwamba. Naam. Katika Waefeso 5:26, njia pekee unayoweza kupitia kwenye Mwamba huo, hiyo ni, "Kuoshwa kwa maji ya farakano kwa Neno." Hiyo ni kweli.

165 Sasa, usiache ibilisi huyu akunyunyizie elimu yake. La, la. Itaua ushawishi wako. Usiache ibilisi achukue hiyo, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa ambalo mama yangu alishiriki, ambalo baba yangu, nyanya yangu." Usiache ibilisi akunyunyizie hilo. Biblia imesema tayari, kwenye Nyakati Saba za Kanisa, na vitu hapo, yote yamekauka! Hiyo ni kweli. Kitu hicho chote kimepotoka. Kitu hicho chote ni jeraha lenye usaha. Usimwache akunyunyizie, useme, "Vema, ni maadili ya juu zaidi. Sisi tuna elimu zaidi kuliko tulivyokuwa katika siku za kale." Usimwache ibilisi aweke hilo juu yako. Nimekuonyesha utaratibu wake wote wa ustaarabu, elimu na sayansi. Ameuingiza moja kwa moja ndani ya kanisa, wala msisikilize hayo. Ondoa kichwa chako kutoka maskini televisheni hizo chafu na kadhalika!

166 Nalo somo letu linasema, "Msifuatishe namna yake, bali mgeuzwe." Sio kuingia na kusema, "Nilipewa kipa imara, Jumapili." La. Ingia ukageuzwe sasa, ukageuzwe kutoka jinsi ulivyo, upate kuwa jinsi Mungu anavyokutaka uwe.

167 Sasa, inategemea ni mbegu ya aina gani iliyo ndani yako. Kama mbegu ya kiakili, ya kielimu imewekwa ndani yako, kuna jambo moja tu inaloweza kufanya, kukuumbua, hivyo tu, kwa mwana ama binti ya Mungu. Ndilo jambo pekee inaloweza kufanya. Watu siku hizi, ninapoangalia nje, wanatenda kana kwamba hata hawaamini Mungu yupo.

168 Samahani tamshi hili. Kama mtu yeyote anajisikia kuumizwa na hili, silimaanishi. Jumapili kadhaa zilizopita nilialikwa, na binti yangu mwenyewe, kuja kwenye televisheni nikaangalie nyimbo za dini. Ni kwenye Jumapili asubuhi. Nilitaka kumsikiliza Oral Roberts katika kipindi chake, nikawaambia wanijulishe. Kasema, "Hebu usikilize huu, huu ni wimbo mzuri sana wa kidini, unaoimbwa." Mwanangu akisimama pale, akaniambia juu yake, pia. Ndipo nikaifungulia hiyo . . .

169 Tumekodi kutoka kwa mwanamke aliye na televisheni nyumbani mwake. Kamwe sikusudii kuwa na moja nyumbani mwangu. La, bwana. Sikitaki kitu hicho nyumbani mwangu. Ningekipiga risasi kwa bunduki yangu ya marisau. Sitaki

uhusiano wowote na kitu hicho kiovu. La, bwana! Lakini nikachukua ninii . . .

170 Hebu niwaambie juu ya ninyi Waarizona hapa. Mliona ule mchanganuo hivi majuzi, wa shule, sivyo? Asilimia themanini ya watoto kwenye shule za Arizona wanaugua upungufu wa akili, asilimia sitini na saba wa hao ni kutokana na kutazama televisheni. Vipi kuhusu hilo?

171 Afadhali ukaitumie bunduki yako ya marisau! Mnaona? Sasa, usimwache ibilisi akunyunyizie hilo. La, bwana. Sasa ninyi watu, kama nilivyosema, watu wanatenda kana kwamba haiwabidi kuja Hukumuni.

172 Hawa wavulana na wasichana, walikuwa na familia ya Kihindi, na upuuzi mwingi sana. Nafikiri jamaa mmoja jina lake Bw. Pool ndiye kiongozi wake. Na kama nilipata kuona dhihaka mamboleo ya nyimbo za dini, ilikuwa ni jinsi walivyokiendeleza; kundi la akina Ricky wamesimama pale, wakitikisa mikono yao juu chini.

173 Hakika nilipendezwa na yule kijana hapa asubuhi ya leo, aliyeimba, alionekana mstahifu, kama mwanamume halisi. Na—napenda hilo. Wakati ninyi—ninyi wafanya biashara hapa mnapolipata kundi la hawa akina Ricky wanaosimama hapa, na kupiga makelele na kupaza sauti, na kufanya yasiyofaa, na kushikilia pumzi zao hata wanakuwa bluu usoni; na huko si kuimba, huko ni kupiga tu kelele nyingi sana za kisayansi. *Kuimba* ni "sauti tamu ya kutoka moyoni."

174 Ndipo nikawazia, "Huzuni jinsi gani! Ni aibu jinsi gani! Kwa hiyo ni vipi chini ya jina la dini, wao wanatenda kana kwamba hakuna Mungu!" Mtu fulani alisema, hivi majuzi, akamwambia mvulana anayeenda na binti yangu. Mvulana Mkristo alisema, alitoa tamshi la kielimu kuhusu Adamu na Hawa, kasema, "Hawa akipitia bustanini. Kasema, 'Enyi watoto, mnaona ule mti pale?' Kasema, 'Hapo ndipo mama yenu alitufukuza nyumbani na makazini.'" Ungeweza kuwazia, anayedhaniwa ni Mkristo hodari, ambaye angechukua ahadi na Neno la Mungu na kuitupa kwenye kizimba cha nguruwe! Wanatenda kana kwamba haiwabidi kuja Hukumuni. Bali Mungu ataleta kila siri Hukumuni. Wanatenda kana kwamba hakuna Mungu.

175 Sitaki kuwaita pumbavu, kwa kuwa Biblia ilisema . . . pumbavu, sio sawa. Yesu alisema si sawa. "Usimwite mtu yeyote mpumbavu." Lakini katika Zaburi 14:1, "Mpumbavu alisema moyoni mwake, 'Hakuna Mungu.'" Mnaona? Hao, hawaninii . . . Sitaki kuwaita wapumbavu, lakini wanatenda kana kwamba ndivyo walivyo. Wanatenda jinsi hiyo.

176 Kwa hiyo, unaona mahali tulipo leo hii, kama, "Hakuna Mungu." "Mimi ni mfuasi wa kanisa!" Nao wote, jambo lote, Biblia, ni mzaha mkubwa. "Kanisa letu linajua mahali wanakoenda!" Naam . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .

moja kwa moja mpaka kuzimuni, kweli kabisa. Moja kwa moja njiani mwao, moja kwa moja kupitia sayansi na elimu, seminari za kitheolojia na kadhalika, zikiwapeleka upesi moja kwa moja barabarani. Roho Mtakatifu hana nafasi ya kutoa ufunuo wala chochote kile; seminari tayari imeyapanga yote.

177 Roho Mtakatifu anapaswa kutuongoza; sio seminari, sio maaskofu na wasimamizi, na kadhalika. Roho Mtakatifu Ndiye Kiongozi wetu.

178 Kaini alikuwa ni mtu kama huyo. Alikuwa ni wa kidini kwelikweli. Sasa, kama dini ndiyo yote unayopaswa kuwa nayo, basi Mungu hakuwa na haki ya kumhukumu Kaini. Kwa sababu, yeye alikuwa ni wa kidini, alikuwa ni wa kidini tu na mwaminifu jinsi Habili alivyokuwa. Sasa kumbukeni, yeye alimwazia Mungu, alimwabudu Mungu, alikuwa na kanisa, alijenga madhabahu, alitoa dhabihu, akaomba, akaabudu, bali alikataliwa. Haidhuru ni jinsi gani. . .Esau alikuwa hivyo, pia. Mnaona?

179 Dini, mnaona, hiyo ni kazi ya Shetani; sio kuua kitu hicho chote, bali kukiambukiza tu. Hivyo tu. Hatakiua kitu hicho chote. Loo, sio wakomunisti; la, la, upinga Kristo sio ukomunisti. Biblia ilisema, "Itawapoteza walio wateule kama yamkini." Msiliangalie pazia la chuma, bali la zambarau. En-he.

180 Lakini, angalia, Kaini alikuja kuabudu, bali alikuwa na mbegu mbaya ndani yake, uzao wa nyoka. Mlio wa nyoka ulikuwa umelia juu yake, kwa kuwa yeye alikuwa ni uzao wa mwanamke. Alijua mapenzi makamilifu ya Mungu, bali akakataa kuyafanya. Mlijua hivyo? Shetani anajua mapenzi ya Mungu, bali anakataa tu kuyafanya.

181 Angalia, alikuwa amemwona Mungu akiuthibitisha ujumbe wa Habili. Sasa ninawatakeni muwazie, tumieni Chujio lenu la mtu mwenye busara sasa kwa dakika moja. Ujumbe wa kweli wa Habili, ambao Mungu aliuthibitisha kwamba ni Kweli! Mnavuta sasa? En-he. Ujumbe wa Habili ulikuwa umepokelewa, naye Kaini akauona na akajua ya kwamba Mungu alikuwa ameuthibitisha ujumbe huo kwamba ni wa kweli. Lakini kamwe asingeweza kufanya hivyo. Kiburi chake kilimzuia. Hiyo ni kweli, kiburi chake kilimzuia asifanye hivyo. Alimwona Mungu akiuthibitisha ujumbe huo.

182 Ndivyo inavyoonekana sasa, ni vigumu sana kwa watu kujinyenyekeza kwenye Neno la Mungu. Wao, wao hawataki kufanya hivyo. Watajinyenyekeza kwenye kanuni za imani za kanisa, hakika, bali si kwa Neno la Mungu.

183 Kama mkitaka kuona jambo hili, nendeni kwa. . .Ninayo Maandiko hapa, hayo ndiyo ninayorejea hapa. Mwanzo 4:6 na 7, Mungu alimwambia Kaini, kasema, "Kwa nini uso wako umekunjamana? Kwa nini umejaa hasira hivyo, ukienda huku na huku? Ndio kwanza usikie ujumbe uliokufadhaisha." Kasema,

"Vema, unafanya hivyo kwa sababu gani? Kwa nini uso wako umekunjamana, ni kwa sababu sikuja kanisani mwako? Basi kwa nini ukafanya hivyo?"

Je! mnatumia Chujio la mtu mwenye busara? Mnaona?

184 Ama, "Kwa nini hukuninii . . . Kwa nini unaonekana hivyo?" Kasema, "Kama utafanya vema, nenda ukafanye kama ndugu yako anavyofanya huko nje, nitakupokea na kukubariki. Nitakufanyia jambo lile lile." Lakini kamwe asingeweza kufanya hivyo. Yeye alisema, "Sasa, usipofanya hivyo, dhambi ya kutokuamini inakuotea mlangoni."

185 Sasa wakati wanapotwambia, "Siku za miujiza zimepita," wanaiona ikithibitishwa na kuhakikishwa kikamilifu sana, mnaona, mambo haya yote ambayo Mungu aliahidi angeyafanya katika siku za mwisho, ya Ufunuo 10 na Malaki 4, mambo hayo yote yakithibitishwa kikamilifu sana, kuna shida gani, ndugu? Kuna shida gani, mnaona?

186 Wasipoamini; kutokuamini, ambako ni dhambi. Kuna dhambi moja tu, hiyo ni, kutokuamini. Hiyo ni kweli. Huhukumiwi ati kwa sababu unakunywa pombe, kuvuta sigara, kutafuna, kuvaa kaptura, kufanya chochote unachofanya. La, hilo halikuhukumu. Ni kwa sababu huamini. Ungaliamini, usingefanya hivyo. Unaona? Mwaminio hafanyi hivyo. Yeye huchukua Chujio la mtu mwenye busara, mnaona, mnaona, ama Chujio la mwanamke mwenye busara, mmojawapo. Vema. Lakini, unaona, dhambi imo mlangoni.

187 Sasa angalia kile hilo lilichomfanyia Kaini, na itakuwa vivyo hivyo leo hii. Lilimfanya Kaini aondoke, mtenda dhambi makusudi. Alikataa kutii makusudi. Kila mtu atakuwa vivyo hivyo. Kutokutii makusudi baada ya kuona ujumbe wa Habili ukithibitishwa na Mungu, kwamba ulikuwa ni wa kweli, naye akakataa kutii. Alifanya vivyo hivyo wakati huo. Ndipo akavuka mpaka.

188 Upo mpaka mnaoweza kuvuka. Mnajua hivyo, sivyo? [Kusanyiko linasema "Amina."—Mh.] Sasa, wahudumu, hapa pamoja na huko nje kwenye—kwenye mtandao wa simu ambako matangazo haya yanapitia nchini, hivi mnatambua hilo? Mnapoona ni Maandiko, wala hamtayatekeleza, Mungu daima hataninii . . . Ataninii . . . Loo, mtaendelea, mbarikiwe. Vivyo hivyo kila mmoja wa Israeli, waliishi moja kwa moja nyikani, na kuwalea watoto, mimea, na kubarikiwa, na kila kitu, lakini "kila mmoja wao ametengwa milele na Mungu." Yesu alisema hivyo. Loo, naam, Mungu ataendelea kukubariki, bali umekwisha. Hakika. Hivyo ndivyo Biblia inavyosema sasa, hivyo ndivyo Yeye alivyosema. Angalieni, unaweza kuvuka mpaka. Unaamini hilo? ["Amina."] Kaini aliuvuka.

189 Hebu—hebu tufungue tu hapa kwa dakika moja, nina Waebrania 10:26. Hebu tuone kama ninaweza kupapata hapo

upesi sana. Kitabu cha Waebrania, mlango wa 10 na ninii . . . Ninaamini, kifungu cha 26. Nimekiandika hapa. Hebu kidogo tu, kama mtanivumilia, na hebu tupasome kwa dakika moja. Vema, hiki hapa.

> *Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya . . . kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya* dhambi*;*
>
> *Bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao* wapingao.

190 Hiyo ni NENO TAKATIFU LA MUNGU LASEMA HIVI. Kama tukikataa kuamini kusudi tukiisha kuliona na kulisikia, basi tumevuka mpaka. Kamwe hakutakuwako na msamaha wowote tena kwa hilo, umekwishavuka mpaka.

"Loo," mnasema, "Mungu angali ananibariki." Loo, naam.

191 Kumbukeni Israeli, wale wakwamia mpakani. Mungu alipowapa ahadi, kwenye Nchi Takatifu; nchini, ilikuwa ni nzuri, ya maziwa na asali. Na wakati Musa alipowatuma Kalebu na Yoshua, na wale wapelelezi, kwenda huko na kuipeleleza nchi hiyo, na kuleta ushahidi uliothibitishwa.

192 Kumi kati ya hao walisema, "Hatuwezi kufanya hivyo. Hatuwezi. Angalieni shida huko. Tutakuwa ni walokole. Tuna vitu hivi vidogo vya kupigania vita. Angalieni walivyo navyo. Sisi, hatuwezi. Hatuwezi kuiteka."

193 Yoshua na Kalebu wakasema, "Sisi tunaweza kuiteka hata na zaidi! Mungu alifanya ahadi."

194 Na, kumbukeni, walirudi nyuma. Hiyo ilikuwa ni huko Kadeshi-barnea. Nao walirudi nyuma wakawa wazururaji nyikani. Na kila mmoja wao akafa, na amepotea Milele. Yesu alisema hivyo.

195 Usivuke mstari huo wa kutenganisha, unaona. "Unapojua kufanya mema, na usifanye, kwako ni dhambi."

196 Israeli walifanya jambo lile lile. Baada ya kumwona Musa amethibitishwa, kisha wakamwacha Balaamu awanyunyizie, ile Mbegu ya thamani iliyothibitishwa. Mchungaji, (kamwe) usiseme kitu dhidi ya Neno hili. Mwangalie Balaamu, yeye alikuwa ni nabii, naye aliiona Mbegu ya Mungu ikithibitishwa. Lakini chini ya dhehebu lake kuu alimoishi, Moabu waliona kundi hilo la wazururaji likipitia nchini, akalinyunyizia, na kusema, "Vema, ngoja kidogo. Sisi sote ni Wakristo. Sisi sote ni waaminio. Mbona, baba zetu na baba zenu ni mmoja. Hivi sisi si watoto wa Lutu? Hivi Lutu hakuwa binamu wa Ibrahimu? Hivi sisi sote si kitu kimoja? Hebu na tuoane." Nao Israeli, kama vile Hawa katika bustani ya Edeni, alivyomwacha Shetani amnyunyizie, yeye pia aliwanyunyizia Israeli kupitia nabii wa uongo. Wakati, nabii halisi alikuwa pamoja nao, pamoja na Neno lililothibitishwa. Lakini kwa dhana za maarifa ya kielimu,

yeye aliwanyunyizia. Wazia hilo. Sasa, kamwe haikusamehewa, dhambi hiyo kamwe haikusamehewa.

197 Hizo mbegu zilioza moja kwa moja wakiwa kazini, wakienda zao kwenye nchi ya ahadi. Kila mmoja wao aliangamia na kuoza, moja kwa moja kanisani, wakiwa kazini, wakimfuata Mungu. Na kumwacha Shetani awanyunyizie nyunyizo hilo la kiakili, dhana hiyo ya kielimu, kiakili, akisema, "Mbona, sisi sote ni sawa, sisi sote ni wana wa Mungu." Sivyo! Bali alimwacha mwalimu huyo wa uongo pale awanyunyizie hiyo dhana ya kiakili aliyokuwa nayo kulihusu.

198 Na kama vile tu lile Baraza la Ekumeni linavyofanya sasa hivi, mnaona, jambo lile lile, "Mbona, sisi sote tutaungana pamoja katika shirika moja kuu." Mfumo wenu wote wa kimadhehebu ni wa ibilisi. Ndio alama ya mnyama, katika Biblia. Nitakuwa na kitabu juu ya jambo hilo, hivi karibuni, Bwana akipenda.

199 Angalia, katika wakati wa Nuhu, wakiliona Neno likisimamishwa, lipate kuelea. Sasa hebu nitoe tamshi dogo hapa, Neno likiwekwa pamoja kwa ajili ya kugeuzwa kutoka ardhini hadi angani. Wakiona muundo wa kitu hicho; bali kwa dhana zao za kiakili, walicheka usoni pa nabii, Nuhu, wakati alipokuwa akitabiri juu ya wakati wa mwisho. Lakini alininii . . . Chombo hicho kilifanywa kwa Neno la Mungu, kikatiwa lami ndani na nje, kwa maombi na imani. Wakati mvua ilipokuja, dhana zote za kiakili za dini zilikufa na kuoza moja kwa moja katika ninii . . . moja kwa moja makanisani mwao, moja kwa moja juu ya nchi. Nayo safina ikaelea juu ya yote. Mbegu iliyonyunyiziwa kisayansi ikaozea kwenye hukumu.

200 Tunajaribu kufanya nini, kwa vyovyote vile, je! tunajaribu kuimarisha kanisa letu ama tunajaribu kuimarisha Neno la Mungu? Tunajaribu kufanya nini? Tunashughulikia kitu gani? Tunajaribu kuwarudisha watu kwenye Hili? Huyu Hawa mashuhuri anajaribu kufanya nini hapa katika siku hizi za mwisho, hili kanisa Hawa?

201 Itanibidi kuondoka mara moja, ndugu, maana ina—inachelewa sana. [Ndugu fulani anasema, "Endelea!"—Mh.] Nipeni tu yapata dakika kumi na tano zaidi, nami nitasimama kwenye Maandiko ya—yangu hapa. ["Hakika, endelea."] Naam. Vema. Ninajua. Vema, watu labda wanataka kuingia humu na kupasafisha. Lakini naona tu kama ni vigumu kwangu kuondoka. ["Endelea tu." "Vema, hamna haraka."] Nitaharakisha. Vema.

202 Angalieni, yule Hawa mkuu wa kisayansi, wa kielimu, wa kichotara siku hizi, anayeitwa kanisa, yeye anajaribu kufanya nini? Je! anajaribu kulikweza Neno la Mungu, na kuwaacha watu wafanye jinsi wafanyavyo? Hawatumii Chujio la mtu mwenye busara, ama, Chujio la Mungu. Angalia kile wanachozaa.

Wanajitukuza wenyewe. Kanisa linajitukuza, katika mbegu yake iliyoumbuka ya utaratibu wa maarifa, limeifanya jamii nzima kuwa jinga kisayansi kwa Neno la Mungu. Sasa nitayashika matamshi hayo, sitayashikilia kwa muda mrefu sana sasa, nimalizie. Jinga kisayansi! Wakati Mungu, papa hapa duniani, anafanya mambo anayofanya, kwa Neno Lake la ahadi, nao wanalipuuza na kuondoka kwa sababu wao ni wajinga kisayansi. Wajinga kisayansi!

203 Nilikuwa nikitabasamu wakati huo kwa sababu ya Ndugu Williams hapa, aliandika hapa kwenye kipande cha karatasi, "Unaweza kuendelea nalo alasiri nzima," kitu fulani. Lakini, ninafurahia hilo, hilo ni zuri kweli. Mnaona?

204 Lakini watu wana—wanatenda dhambi makusudi. Imeleta m—mfumo wote wa ulimwengu wa kanisa siku hizi katika dhambi ya makusudi dhidi ya Mungu. Mbona, uadilifu wa kawaida utawathibitishia ya kwamba ni kweli. Vema. Pazia la tamaa mbaya iliyapofusha macho yake, kwa Neno la Mungu, naye anajikuta uchi tena. Mnajua, Mungu, katika Ufunuo 3, alisema, "Njoni, mnunue dawa ya macho Kwangu, macho yenu yapate kufumbuliwa." Mnaona, dawa ya macho ni Neno Lake.

205 Mnajua, wao wanasema, "Vema, mtu huyu alisoma kwa muda wa miaka arobaini, kupata digrii zake. Yeye ni B.L.D., D.D., na yote haya."

206 Mnajua yale Yesu aliyosema kuhusu hilo? Alisema, "Mtu na ajikane mwenyewe." Paulo alisema.

Unasema, "Hilo halimaanishi hivyo."

207 Vema, kwa nini Paulo alilifuatilia, basi? Yeye alisema, "Sikuja kwenu kwa maneno ya kuvutia akili za hekima ya mwanadamu, kwa sababu mngejenga matumaini yenu juu ya hiyo. Lakini niliwajia kwa nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu, neno lenu lipate kuwa . . . imani yenu ipate kujengwa juu ya Neno la Mungu, sio madhihirisho ya hekima."

208 Inaonekana kana kwamba watu wamepoteza uadilifu wao wa kawaida na adabu. Hawako jinsi walivyokuwa. Ilikuwa kwamba, wakati nabii aliposema, "BWANA ASEMA HIVI," watu walitetemeka. Naam, hakika walitetemeka. Watu waliondoka, kwa kuwa waliogopa. Lakini sasa walipoteza hofu yao yote juu Yake. Hawamchi Mungu.

209 Sulemani alisema, "Ku—kumcha Mungu ndio chanzo cha hekima," chanzo chake tu.

210 Lakini nabii anaweza kusema BWANA ASEMA HIVI; watu waseme, "upuuzi!" Mnaona, hakuna tumaini kwao. Ni, wao wanasema, "Mbona, sisi ni werevu. Sisi ni wenye akili, si lazima tuchukue upuuzi wa namna hiyo! Tunajua kile tunachozungumzia!"

211 Pia ni methali ya kale, ya kwamba, "Wapumbavu watatembea kwa viatu vya njumu, ambapo Malaika wanaogopa kukanyaga." Hakika.

212 Sasa, kugeuza ni kitu gani? (Upesi.) Tunakupataje? Ni kitu gani kinachogeuza? Mungu hufanya hivyo kwa Roho wa Neno Lake. Yeye hugeuza. Yeye hupanda Mbegu Yake, akaitupa Roho Yake Kwake, Nayo inazaa mazao. Roho Wake Mtakatifu huligeuza hilo Neno Mbegu lipate kuthibitishwa kwa jinsi yake.

213 Aina ya mbegu uliyo wewe, hiyo inaonyesha ni kitu gani kilicho ndani yako. Huwezi kuificha. Chochote ulicho ndani, kinaonekana nje. Huwezi kuizuia kamwe. Huwezi kuufanya ule mti chochote ila kile ulicho. Unaona, u—utakuwa hivyo. Roho Makatifu huzigeuza mbegu zilizo ndani yake. Haidhuru ni mbegu ya namna gani, litaigeuza. Kama ni ovu, itazaa uovu. Kama ni nafiki, itazaa mnafiki. Kama ni Neno halisi la Mungu, litazaa mwana halisi na binti halisi wa Mungu, kupitia Chujio la mtu mwenye busara. Wakati hiyo Mbegu inapochipuka, hupitia kwenye Hilo, inazaa mwana na binti ya Mungu.

214 Siku moja wakati ulimwengu ulikuwa katika giza la machafuko, Mungu...Sasa sikilizeni kwa makini, maana hatutazungumza...muda kidogo tu zaidi. Angalieni. Siku moja ulimwengu ulipokuwa katika kila namna ya dini tena, kuosha mikono, vyungu, kuvaa mavazi mbalimbali na kofia, na kadhalika, ulikaa katikati ya machafuko mabaya sana. Israeli wa kweli wa Mungu walikuwa wamepotoshwa sana kutoka kwa sheria na maagizo ya Mungu, Yesu alisema, "Ninyi, kwa mapokeo yenu, mnalitangua Neno la Mungu kwa watu, kwa mapokeo yenu." Basi waangalieni hao makuhani watakatifu, walivyowaita; naye Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mtafanya." Mnaona, hivyo ndivyo alivyosema hasa.

215 Sasa wakati ulimwengu ulikuwa katika hali kama hiyo, Roho wa Mungu alitulia tena juu ya Mbegu iliyokusudiwa tangu zamani. Akafasiri na kugeuza Isaya 9:6 ya ahadi Yake; Yeye, Mungu, alifanyika katika mwili wa mwanadamu, kuuokoa wakati huo wa machafuko. Wakati mwanadamu alipofanywa katika sura ya Mungu, huyu hapa Mungu anakuja, kwa kuona awali kwa nabii...Sasa kumbukeni lile Neno, nabii aliliona awali, nabii yule yule aliyemwona Shetani katika siku hizi za mwisho, mnaona, juu ya utaratibu huu wa elimu na vitu alivyo navyo, utaratibu wa dini. Nabii yule yule, Isaya 9:6, alisema, "Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto mwanamume; na Jina Lake ataitwa 'Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele.' Na utawala Wake hauna mwisho." Nalo Neno hilo ni Neno la Mungu. Naye Roho akatulia juu ya hilo Neno, nalo likaumbika katika tumbo la bikira; Mwanadamu, "Mwana amezaliwa," sio kuumbwa, "kuzaliwa."

216 Shetani alijaribu na kujaribu tena, kulinyunyizia. Yeye alimpandisha juu na kusema, “Kama Wewe u vile unavyosema ulivyo, basi fanya baadhi ya uponyaji huu hapa kwa ajili yangu. Nionyeshe jinsi unavyoweza kuufanya. Geuza huu, mkate, na mawe haya yawe mkate. Hebu tukuone ukipiga mbizi, kwa kuwa Maandiko yanasema Wewe utafanya hivyo.”

217 Mnawaona hao pepo wa kidini siku hizi wakiwa wangali wanasema jambo lilo hilo? “Kama kuna kitu kama uponyaji wa Kiungu; huyu hapa Ndugu *Nanii* amelala, hebu tukuone ukimponya.”

218 Pepo yuyo huyo alisimama msalabani mwa Yesu, kasema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka msalabani.”

219 Neno lilisema Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Roho alithibitisha Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Isaya 9:6 ilitimizwa. Na hivi majuzi usiku, wengi wenu katika matangazo mlisikia jinsi tulivyotoa karibu Maandiko sitini na kitu, ninaamini, kuhusu kuthibitisha ya kwamba Maandiko yalisema ya kwamba Huyo alikuwa ni Yeye.

220 Loo, Shetani alijaribu na kujaribu tena, kufanya kila kitu. Usiku mmoja, akiwa amelala nyuma ya chombo, yeye alimwona amelala. Ndipo akasema, “Nitamwangamiza sasa hivi.” Bali asingeweza.

221 Yeye alijaribu kumjaribu afanye mabaya, bali asingeweza kufanya hivyo. Kwa nini? Alikuwa amenyunyiziwa kifukuzi cha kuchaguliwa tangu zamani. Hakiwezi kudanganywa. La, la. Neno lilisema Yeye angekuwa hapa. Amina. Hakuna ibilisi atakayemsumbua, wala hakuna mwana mwingine wa Mungu, ambaye amechaguliwa tangu zamani kupachukua mahali pake. Yeye amenyunyiziwa kifukuzi. Sumu ya Shetani, madaktari wa kimadhehebu hata hawamgusi hata kidogo. Yeye anaenda moja kwa moja, hakuna cha kumsumbua, mnaona. Hakikuwa na athari yoyote juu Yake.

222 “Vema, nitakufanya askofu wa dunia nzima. Ninaitawala. Kama tu utaniabudu, njoo ukajiunge na kundi langu, ni—nitakufanya mtawala. Nitashuka, nikuache utawale.”

223 Yeye akasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani. Imeandikwa, ‘Utamsujudia Mungu, Neno, na kumwabudu peke Yake.’” Ndipo siku moja . . .

Juu ya Mtu huyu mkuu, ningetaka kukaa hapo kidogo.

224 Lakini siku moja, Roho akatulia juu Yake tena; maana kulikuwako na Neno fulani lililokuwa limeandikwa kumhusu Yeye, lililotoka kwa Mungu, kwa njia ya nabii, “Naye aliongozwa machinjioni, kama mwana-kondoo.” Ndipo Roho akatulia juu Yake, na kumwongoza, na kumpeleka kwenye msalaba wa Kalvari. Hapo akafa. Na kila kitu kilichonenwa juu Yake katika mauti Yake, kilitimia, kuleta Nuru na Uzima kwa Mbegu yote

ya Mungu iliyokusudiwa tangu zamani iliyokuwa juu ya nchi. Yeye alileta njia ya kufanya hivyo. *Hii* hapa ile Mbegu, Roho analeta Uzima; akiwageuza wana na binti za Mungu, kutoka kwa ulimwengu katika machafuko haya yenye giza, wakawa wana na binti za Mungu.

225 Msikwazwe na hilo neno "kuchaguliwa tangu zamani." Ninajua mnakwazika. Lakini, sikilizeni, Hilo si neno langu. Ni moja la Maneno ya Mungu. Mkitaka kulisoma, someni Waefeso 1:5, ambayo, "Yeye alitangulia kutuchagua ili tuwe wana kwa njia ya Yesu Kristo." Mnaona?

226 Hebu tu nilifafanue kwa dakika moja tu, dakika moja tu, kuvunjilia mbali hili kutoka niani mwenu. Angalia. Kama tu vile wewe ulivyokuwa katika baba yako, hapo mwanzo, chembe hai. Je! mlijua hilo, kila mmoja wenu? Ulikuwa katika babu wa babu wa babu wa babu wa babu yako, pia, je! mlijua hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

227 Hebu someni Kitabu cha Waebrania, ambamo tunaona ya kwamba Lawi alitoa zaka wakati alipokuwa kwenye viuno vya Ibrahimu, vizazi vinne nyuma yake. Wakati Ibrahimu alimpa Melkisedeki zaka, ilihesabiwa kwa huyu mjukuu wa mjukuu wa mjukuu wake chini yake, na wakati huo alikuwa viunoni mwa Ibrahimu. Haya basi. Mnaona?

228 Wewe ulikuwa katika viuno vya baba yako, bali baba yako asingeweza kufanya ushirika nawe mpaka ulipogeuzwa ukawa mwili wa nyama.

229 Mwanangu pale alikuwa ndani yangu. Ni—ni—nilitaka mwana, bali alikuwa yu ndani yangu wakati huo. Mnaona? Alikuwa ndani yangu wakati huo. Lakini kwa njia ya ndoa, aligeuzwa akawa mtu kama mimi, ndipo akawa kama nilivyo mimi.

230 Nawe unakuwa kama wazazi wako, unaona, maana ilikuwa ndani yako, kwanza kabisa. Sasa kama sisi ni wana wa Mungu, sifa Zake . . . Ambapo, wewe ni sifa ya baba yako, sio mama yako; baba yako. Chembechembe hai hukaa ndani ya baba. Mnaona? Na sasa mama yako alikuwa ni kiangua mayai kilichokubeba, kilichoibeba mbegu ya baba yako. Unaona?

231 Na dunia, katika mwili, pia ni kiangua mayai kinachoibeba mbegu ya Mungu. Mnaona, kweli kabisa. Sio ulimwengu, jinsi ulimwengu ulivyo mkuu; ni jinsi Mungu aliyeuumba alivyo mkuu. Mnaona? Mnaona?

232 Sasa kama wewe ni mwana ama binti ya Mungu, basi ulikuwa katika Mungu hapo mwanzo. Wewe ni sifa Yake. Kama hukuwa huko wakati huo, basi kamwe hukuwako wala kamwe hutakuwako.

233 Maana, siwezi kuzaa, kutoka viunoni mwangu, mwana wa mtu huyu *hapa* ama mtu yule *pale*, ninaweza tu kuwazaa

wanangu mwenyewe, nao watachukua sura yangu. Haleluya. Mnaliona?

234 Wana na binti walikuwa ndani ya Mungu hapo mwanzo. Sasa angalia. Unao Uzima wa Milele, unasema. Tunaamini, kwamba tunao Uzima wa Milele. Vema, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na hiyo ni Mungu. Hicho ndicho kitu pekee kilicho cha Milele, ni Mungu. Ndipo kama unao Uzima wa Milele, Uzima huo ulio ndani yako ulikuwako daima, nawe ulikuwa kwenye viuno vya Mungu kabla hata hapajakuwapo na ulimwengu. Na wakati Neno Lenyewe . . . Yesu Mwenyewe anaitwa Neno, na katika Yohana Mtakatifu 1, ilisema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, na Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa ni Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Basi ulikuwa viunoni mwa Yesu, nawe ukaenda Kalvari pamoja Naye. Ukafa pamoja Naye, nawe ukafufuka pamoja Naye. Na leo hii tumeketi katika ulimwengu wa Roho ndani Yake, tumejazwa na Roho Wake, wana na binti za Mungu. Tukafa pamoja Naye, tukafufuka pamoja Naye. Hakika.

235 Sasa basi, sasa, sasa unaweza kufanya ushirika pamoja Naye. Usingeweza huko nyuma, kwa sababu ulikuwa ni Neno tu ndani Yake, mbegu. Lakini sasa Yeye amekudhihirisha, na sasa Yeye anataka ushiriki pamoja Naye. Ndipo akashuka, akafanyika mwili kusudi aweze kushiriki kikamilifu pamoja nawe. Mnaona ushirika huo mkamilifu? Loo, jamani, hizo siri zenye kilindi za Mungu! Ni ajabu jinsi gani! Mnaona, Mungu asingeweza kushiriki katika Roho, kwa hiyo Mungu akawa mwanadamu pamoja na sisi.

236 Yesu Kristo alikuwa ni Mungu Mwenyewe, aliyedhihirishwa, maana, Yeye alikuwa Mwana kwa sababu alizaliwa, bali ilikuwa tu ni maskani apate kuishi humo. "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote, bali Mzaliwa pekee wa Baba amemfunua." Mungu alijijengea nyumba, mwili wa kuishi ndani, akashuka upate kumgusa. Timotheo wa Kwanza 3:16, "Na bila shaka, siri ya utauwa ni kuu; kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na malaika, akaaminiwa, akachukuliwa Mbinguni." Mnaona? Sasa Yeye . . .

237 Wewe ukiwa katika mwili, na Yeye akiwa katika mwili, basi mnaweza kufanya ushirika sasa, maana Yeye alikuwa ni sifa ya Mungu ya upendo. Mungu ni upendo. Hiyo ni kweli? Naye Yesu alikuwa ni sifa ya Mungu ya upendo. Ndipo hapo sifa ya upendo ilipoonyeshwa, ambayo, huyo alikuwa ni Mungu Mwenyewe; sifa zote ambazo zilimkalia, zilimjia, "Wote alionipa Baba, watanijia Mimi." Hakika, ilibidi watangulie kuchaguliwa. Kama sivyo, wewe hutakuwako. Hivyo tu. Hakika.

238 Sasa tunaweza kushiriki, ilikuwa ni kupitia kwenye u— utajiri wa Neno Lake, na ambalo wewe ni sehemu Yake. Wewe ni sehemu ya Neno; kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno hapo mwanzo,

wewe ni Neno sasa. Unaona? Ninahubiri usiku wa leo, ama Jumapili ama moja ya siku nitakapoingia, kuhusu Neno ni nini, unaona. Na sasa wewe ni sehemu ya Neno.

239 Sikilizeni. Lipo jambo moja nisiloweza kufanya. Siwezi kujivunia wahenga wangu. La, nimepitia kwenye mchafuko mkuu. Baba yangu alikuwa ni Mwairishi. Mama yangu alikuwa ni mwanamke wa Kihindi, nusu Mhindi; mama yake alikuwa ni Mhindi, alipata malipo ya uzeeni. Sasa, wote hao, walevi, karibu wote walikufa wamevaa viatu, wakipigana, waliopigana kwa bunduki, na kadhalika. Siwezi kujivunia kitu chochote kuhusu hilo, kwa kuwa wahenga wangu na ukoo wa familia yangu ni mbaya sana.

240 Lakini, ndugu, lipo jambo moja ninaloweza kujivunia, ninaweza kujivunia Bwana wangu Yesu ambaye amenikomboa. Na kwa nguvu Zake za kugeuza akapanda mbegu, kwa kuchaguliwa tangu zamani, nami nikaona. Mimi ni mwana wa nani sasa? Naam. Ninaweza kumjivunia. Nami nimetumia miaka thelathini na mitatu ya maisha yangu, nikimjivunia. Kama angeweza kunipa miaka mingine thelathini na mitatu, nitajaribu kumjivunia zaidi. Mnaona? Ninaweza kujivunia Mhenga wangu, haleluya, Yeye aliyenikomboa na kupanda mbegu ya Uzima *humu* ndani, na kuniruhusu niliangalie Neno hili, akamshusha Roho Wake na kusema, "Hili hapa. Nena *hili*, nalo litatukia. Fanya *hivyo*." Na loo, jamani, ninaweza kumjivunia! Yeye alifanyaje jambo hilo? Kwa kuoshwa kwa maji kwa Neno, maji ya farakano. Laiti tungaliweza kulielezea.

241 Waaminio wa kweli waliochaguliwa tangu zamani watadumu na Neno kwa sababu hao ni sehemu ya hilo Neno.

242 Loo, nyota zinazotangatanga, mtastaajabu kwa muda gani? Ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, walio nje, chochote ulicho, nyota zinazotangatanga, kutoka kanisa hadi kanisa, kutoka kwenye nguzo moja hadi mahali pengine, na televisheni hata kwa televisheni, ulimwengu hadi ulimwengu, mbona msije? Yeye anatamani kufanya ushirika pamoja nawe. Yeye anakutamani. Anataka kukugeuza kwa kufanya upya nia yako, sio kwa kanisa wala dhehebu, bali kwa Neno Lake, ambalo, wewe ni sehemu yake iwapo shauku hiyo imo ndani yako.

> *Heri wenye kiu na njaa* ya *haki; maana hao watashibishwa*. (Mnaona? En-he.)

243 Naye ametuma nguvu Zake za kugeuza, apate kuwatoa katika uumbuaji huu wa dini mliyo ndani yake. Katika mchafuko wa uumbuaji huu tulio ndani yake, Mungu ametuma nguvu Zake za kugeuza, Neno Lake, lililothibitishwa, likahakikishwa, apate kuwatoa kwenye uumbuaji huu wa ujinga wa dini mnaoutembelea, "uchi, kipofu, mwenye mashaka, wala hamjui." Wazieni hilo, enyi marafiki.

244 Mnajua, Mungu alituma nguvu Zake za kugeuza apate kulitimiza Neno Lake, kisha akaubadilisha mwili wote wa Sara pamoja na Ibrahimu. Akamgeuza mzee na bi-kizee, kwa kuwa Yeye aliahidi atafanya hivyo.

245 Na yale Mungu anayoahidi kufanya, hayo Yeye atafanya. Hakuna kitu, kitu chochote. . . Kitu chochote kilichopotoshwa, Mungu hawezi akafanya jambo lolote nacho. Lakini Yeye atalitimiza Neno Lake, Naye atamtuma Roho Wake! "Mimi Bwana nimelipanda. Nitalitia maji mchana na usiku, asije mtu akalitoa mikononi Mwangu." Biblia inasema hivyo.

246 Loo, nyota zinazotangatanga, ninyi mlio na shauku moyoni mwenu! Hamna budi kuwa nayo, la sivyo msingekuwa mmeketi hapa asubuhi ya leo. Wala msingekuwa katika makanisa hayo na majumba ya mikutano, na vitu mlivyomo, huko kote nchini, kama kitu Fulani hakikukuingiza mle. Mtu fulani alinena nawe. Usiende mbali zaidi. Kuna kuoshwa kwa maji kwa Neno, kutakakokufanya mweupe kama theluji. Loo, enyi wana wa Mungu, sikilizeni! Msikae kwenye uumbuaji huo. Ondokeni humo. Ibrahimu alimwamini Mungu, na kuita kila kitu kinyume . . .

247 Unasema, "Nitapataje riziki yangu? Nitafanyaje jambo *hili*?" Hilo ni jukumu la Mungu. "Ningewezaje? Rafiki zangu watanikataa."

248 Mungu alisema, "Yeye atakayemwacha baba yake mwenyewe, mama, mke, mume, makazi, nyumba; nitawapa makazi na nyumba, nitawapa baba na mama, na ndugu na dada, katika ulimwengu huu, na Uzima wa Milele katika ulimwengu ujao." Ni ahadi, ewe rafiki. Hilo, loo, hilo halina budi kumwagiliwa maji! Kila ahadi anayoifanya Mungu hutimia. Kila Mbegu ya Mungu ni ahadi.

249 Na, dada, acha kuzikata nywele hizo, kwa sababu si jambo la kawaida mbele za Mungu. Acha kuvaa nguo hizo, ni chukizo Kwake!

250 Ninyi ndugu, ninyi wanaume, acheni kuyashughulikia madhehebu haya, katika kufanya mambo hayo, na kuwaacha wake zenu wafanye mambo kama hayo. Si vema kwa Mkristo.

251 Rudini kwenye Neno! Lichukueni Neno hilo, litakua. Halina budi kukua. Nguvu za Mungu za kugeuza ambazo zililileta mara ya kwanza, Yeye yuko njiani akirudi, akilirudisha tena. Yeye anarudi tena mahali lilipokuwa.

252 Henoko alihamishwa, kutoka mautini, kwa nguvu za Mungu za kugeuza. Kwa nini Mungu akafanya jambo hilo? Kama mfano wa Kanisa linalonyakuliwa ambalo linakuja. Naam. Eliya alikuwa ni vivyo hivyo.

253 Mwili wa Yesu ulihuishwa baada ya kufa. Na kaburini, mwili wa Yesu ulihuishwa kwa Neno la Mungu; na kugeuzwa, kutoka

kwenye umbo baridi, lililokufa, ukawa ni Mwana wa Mungu aliyefufuka, aliyetukuzwa. Kwa maana nabii, Zaburi 16:10, kama mkitaka kuliandika, 16:10, ilisema, "Sitaiacha nafsi Yake kuzimuni, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Ee Mungu!

254 Hilo Neno halina budi kutimia, ni Neno la Mungu! Lipande moyoni mwako, ikiwa unataka kwenda katika Unyakuo. Ikiwa unataka kuwa Mkristo halisi, liweke Neno hili. Kama ambavyo ninaamini ilikuwa ni Ezekieli, Mungu alisema, "Chukua chuo hicho na ukile," kusudi nabii na Neno waweze kuwa kitu kile kile. Na kila ahadi mle ndani haina budi kujionyesha yenyewe, maana ni Mbegu asili ya Mungu. Msimruhusu mwanatheolojia fulani mwenye elimu hapa nje kusukuma Hiyo kutoka ndani yenu. Msimruhusu awanyunyizie hiyo sayansi na maarifa ya kimwili, na elimu. Mwaminini Mungu!

255 Ibrahimu hakuchukua utafiti wa kisayansi wa siku yake, aseme, "Mimi ni mzee sana kumpata mtoto, nimeenda mbali kupita kiasi. Nimefanya *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*." Lakini aliita chochote kilichokuwa ni kinyume, cha Neno la Mungu, kana kwamba hakikuwa. Wala hakusita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini; bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu. Alijua ya kwamba Mungu angeweza kutenda yale aliyoahidi.

256 Loo, enyi wana wapoteao, walioumbuliwa na vitambaazi vya dunia hii! Dada wapoteao, ambao mahali na mitindo ya ulimwengu huu imewavutia! Na, ewe dada mpendwa, huenda ukanihesabu mzee mwendawazimu, bali moja ya siku hizi wakati utakapokutana na yale Florence Shakarian alikutana nayo hivi majuzi usiku; yeye aliketi kwenye chumba hiki, pia, mahali hapa, kama mjuavyo. Utakapokutana na hayo, utapata kujua, sio mimi, bali Neno hili ni la kweli. Achana na maduka hayo ya kinyozi, maduka hayo ya mitindo. Achana na mambo hayo.

257 Unasema, "Kwa nini usiwafundishe mambo makuu, jinsi ya kuwa *hivi*?" Anzeni tu na ABC zenu, ndipo tutaiendea aljebra. Mnaona? Anzeni tu kusoma, "ndiyo ibada yenu yenye maana."

> *Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.*

258 Ninyi fanyeni tu "ibada yenu yenye maana," Mungu atayashughulikia hayo mengine; mnaona, kuhoji tu mambo unayoweza kuyahoji wewe mwenyewe na kuyafanya. Si ni . . . Si ni kukosa busara kwa mwanamke kujivua nguo, na kutoka hapa nje na kufanya hivyo, wakati Biblia inalihukumu jambo hilo? Si ni kukosa busara kwa mwanamume kujitupilia kwenye fundisho la sharti kama tulivyo nayo siku hizi, na upuuzi huu wote hapa, na upuuzi huu wote wa seminari, na upuuzi kama huo, wakati ni kinyume kabisa na Neno la Mungu? Mnaona?

259 Midomo ya Isaya, yeye alikuwa ni mtu wa kawaida tu mwenye midomo michafu. Yeye alisema, “Bwana, niko miongoni mwa watu wachafu, nami nina midomo michafu. Ole wangu kwa kuwa nimemwona Mungu.” Ndipo Malaika akashuka, akauchukua Moto, Moto Mtakatifu kutoka kwenye madhabahu ya Mungu, naye akaigeuza midomo yake; kutoka midomo ya mtu apoteaye, kuwa midomo ya nabii aliye na BWANA ASEMA HIVI. Nguvu za Mungu za kugeuza!

260 Wavua samaki mia moja na ishirini, na—na maskini wachuuzi wadogo wa zambarau, wa kike, na hao waliokusanyika kwenye chumba cha juu na kuifunga milango, wengine wao bila elimu ya kutosha kuandika majina yao wenyewe. Mungu aliwageuza kutoka kwa wavua samaki, wakawa wavua watu; kutoka kwa wanaume na wanawake mtaani, wakawa watakatifu wa Mungu, wasiopatikana na mauti. Nguvu za Mungu za kugeuza!

261 Paulo, mfuasi wa kawaida wa kanisa, Mpresbiteri, Mmethodisti, Mbaptisti, Mpentekoste, ama yeyote yule; moja kwa moja mtaani alishuka, akiwa na roho yake kuu kaidi, kwamba alijua kuliko yeyote wao. Alikuwa amekulia chini ya Gamalieli, mmoja wa walimu walio bora sana nchini. Ilikuwaje alipokuwa akienda zake Dameski, kulishika kundi la wale waliokuwa wanaliamini Neno la Mungu? Akienda zake kule chini, aliangushwa chini, naye akasikia Ujumbe. Nao ukamgeuza kutoka mfuasi wa kanisa na mwenye kuhudhuria kanisa; akawa nabii wa Mungu, ambaye aliliandika Neno la Mungu, katika Agano Jipya. Kutoka mfuasi wa kanisa akawa mtakatifu!

262 Loo, ewe nyota inayotangatanga, hebu tusitishe. Ewe mwana unayetangatanga, Mbegu ipoteayo inayotangatanga, katika uumbuaji huu; geukeni, asubuhi ya leo, enyi watoto. Naomba mnisikilize kama m—mtu anayejaribu kusimama kati ya walio hai na waliokufa.

263 Huko nje kwenye nchi ambayo matangazo haya yanakuja kama mngali mmeunganishwa, ninyi ambao mmetangatanga mkaingia mahali hapo, naomba mketi tu kwa dakika moja zaidi. Ninajua ya kwamba imechelewa hapa Tucson ama, samahani, Phoenix, ni saa sita kasoro dakika ishirini. Nami nimekuwa na watu hawa hapa asubuhi yote. Nimewatoa kazini mwenu na kadhalika. Lakini angalia, rafiki mpendwa, huenda ukawa mbali na Mungu milele. Naomba urudi asubuhi ya leo. Sivyo? Ipo nafasi kwenye ile Chemchemi.

> Katika hori zamani za kale, ninajua ni kweli kabisa,
> Mtoto Mchanga alizaliwa awaokoe watu na dhambi zao.

Yohana alimwona kwenye pwani, Mwana-Kondoo wa milele,
Loo, Kristo, aliyesulibishwa wa Kalvari.

Loo, nampenda yule Mtu wa kutoka Galilaya, kutoka Galilaya,
Kwa kuwa amenifanyia mambo mengi sana.
Amesamehe dhambi zangu zote, akamweka Roho Mtakatifu ndani;
Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa Galilaya.

Mtoza ushuru alienda kuomba kule hekaluni siku moja,
Akalia, "Ee Bwana, unirehemu!"
Alisamehewa kila dhambi, na amani kuu ikawekwa ndani;
Akasema, "Njoni mmwone Mtu huyu wa kutoka Galilaya." Kweli.

Viwete walifanywa kutembea, bubu walifanywa kuzungumza,
Nguvu hizo zilinenwa kwa upendo baharini;
Vipofu walifanywa kuona, ninajua ingewezekana tu kuwa ni
Rehema ya yule Mtu wa kutoka Galilaya.

264 Linganisha hayo na huduma leo.

Yule mwanamke kisimani, Yeye alitaja dhambi zake zote,
Jinsi alivyokuwa na waume watano wakati huo.
Alisamehewa kila dhambi, na amani kuu ikawekwa ndani;
Akalia, "Njoni mmwone Mtu huyu wa kutoka Galilaya!"

265 Ewe mwanamke, Yeye anaweza kufanya vivyo hivyo. Yeye ameusoma moyo wako asubuhi ya leo. Ewe mwanamume, Yeye ameusoma moyo wako. Loo, ewe mtoza ushuru, na tuombe!

Loo, nampenda yule Mtu wa kutoka Galilaya, kutoka Galilaya,
Kwa kuwa amenifanyia mambo mengi sana.
Amesamehe dhambi zangu zote, akamweka Roho Mtakatifu ndani;
Loo, nampenda, nampenda yule Mtu wa kutoka Galilaya.

266 Hivi hamtampenda, pamoja nami, asubuhi ya leo? Loo, mwenye dhambi mtukutu, anayetangatanga, hapa ama popote ulipo, je! utamkubali Bwana wangu asubuhi ya leo? Yeye ni Neno, Nalo Neno limeletwa kwako. Hivi huwezi kumkubali asubuhi ya leo? Waweza tu kuinua mikono yako ama kusimama

kwa miguu yako, ama kitu kama hicho, na kuomba, useme, "Ninataka kumkubali sasa hivi. Ndugu, niko tayari. Ninataka sasa hivi kumkubali Yeye." Naomba usimame kwa miguu yako, mtu yeyote aliyetaka kuombwa, na kusema, "Mimi . . ." kuombewa, hasa, "Mimi ni mwenye dhambi. Ninataka . . ." Mungu akubariki, bwana. Mtu mwingine? Kila mtu na aombe sasa, kwa dakika moja tu.

Loo, katika hori hilo zamani za kale, (kulikuwa na machafuko, mwajua, ulimwengu ulikuwa umechafuka), nami ninajua ni kweli kabisa,
Mtoto Mchanga alizaliwa awaokoe watu na dhambi zao.
Wakati Yohana alipomwona kwenye pwani, Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo wa milele, (yeye Yule leo)
Loo, Yeye ni Kristo, Aliyesulibishwa wa Kalvari.

267 Hivi hutampenda leo kwa moyo wako wote, upate kutembea utoke kwenye hali hii ya ulimwengu uliyomo? Ninyi wanawake, ninyi wanaume, loo, mliketi hapa wakati huu wote kwa sababu gani? Inaonyesha ya kwamba kuna kitu fulani ndani yenu, kuna kitu mle kinachoona njaa na kiu. Msingeketi hapa saa hizi mbili ama tatu, mkiketi kwenye jengo hili namna hii; kuna kitu fulani. Hivi hamwezi kukiitikia leo hii? Acheni mitindo na sayansi, na mambo yote ya ulimwengu, yaondoke niani mwenu sasa hivi, ndugu mpendwa ama dada mpendwa.

Makanisa yanaungana, mataifa makuu yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara walizotabiri manabii;
Siku za mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
"Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inavunjika kwa hofu;
Jazweni na Roho, zitengenezeni taa zenu ziwe safi,
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

Manabii wa uongo wanadanganya, Ukweli wa Mungu wanaukana,
Ya kwamba Yesu aliye Kristo Ndiye Mungu wetu.

268 Sasa, hiyo ni kweli. Mnajua hilo, sisi sote, siku tunayoishi.

Bali Yeye alisema itakuwa Nuru yapata wakati wa jioni,
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata.

269 Hiyo ndiyo siku tunayoishi sasa hivi. Nuru itaangaza tu wakati wa jioni wakati giza linapoingia, utusitusi wa jioni, ile nyota ya jioni.

> Utusitusi wa jioni na nyota ya jioni,
> Na baadaye giza!
> Naomba kusiwe na huzuni ya kuagana,
> Hapo nitakapoingia chomboni hatimaye;
>
> Kwa kuwa wote walio nje ni mwisho wa majira na wakati,
> Na mafuriko huenda yakanisukumia mbali,
> Bali ninataka kumwona Nahodha wangu uso kwa uso
> Nikiisha kuvuka kile kizuizi.
>
> Usiniambie, kwa hesabu za maombolezo,
> Ya kwamba maisha ni ndoto tupu tu!
> Na nafsi inayolala imekufa,
> Wala mambo hayako yanavyoonekana.
>
> Naam, maisha ni halisi! Na maisha yana bidii!
> Wala kaburi siyo kikomo chake;
> Kwa kuwa u mavumbi wewe, kwa mavumbi utarudi,
> Haikunenwa juu ya nafsi.
>
> Maisha ya watu mashuhuri yote hutukumbusha,
> Nasi tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
> Na, maagano, huacha nyuma yetu,
> Nyayo za miguu kwenye changarawe za wakati;
>
> Nyayo za miguu, ambazo labda mwingine,
> Wakati akisafiri katika maisha haya taadhimu,
> Ndugu mpweke anayeangamia baharini,
> Akiziona, atajipa moyo tena.
>
> Hima, basi, ingia kazini,
> Jiandae kwa shambulizi lolote;
> Usiwe kama ng'ombe bubu, wanosukumwa!
> Kuwa shujaa katika vita!

270 Mungu mpendwa, hao ni Wako. Nimeona wanaume wawili wakisimama kwa miguu yao, Baba. Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utawachukua sasa. Wanataka kuwa wana Wako. Wameamka kutoka kwenye ujinga wa maisha ambayo wameishi, na sasa wanataka kuburudishwa, kufanywa upya, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu juu ya Mbegu hiyo ambayo imepandwa mioyoni mwao leo hii. Mungu wa Milele, Muumba wa vitu vyote, ambaye ulilifanya Neno Lako, nami ninaamini ya kwamba Wewe ulijua watu hawa wangefanya hivi asubuhi ya leo. Ninaomba, Bwana, ya kwamba utalitia maji Neno hilo, usiku na mchana, wala usimwache Shetani alitoe mikononi Mwako. Jalia liwe ni

ule mti ambao siku moja, katika Paradiso ya Mungu, wakati yote yatakaporudishwa tena, kwa kuwa Neno Lako haliwezi kushindwa, litakuwa tena. Kwa kuwa ulimwengu huu . . .

271 Wala hakutakuwako na ustaarabu wa aina hii katika ulimwengu ujao. Hakutakuwako na magari ama chochote ambacho sayansi imepata kufanya. Hakutakuwako na vitu kama hivyo katika ulimwengu ujao. Bali utakuwa ni ustaarabu wa Mungu Mwenyewe ambao atauanzisha katika utawala huo wenye utukufu. Kwa kuwa, katika ustaarabu huu kuna maradhi, mauti, huzuni, makaburi, na mahitaji. Bali kwenye Ufalme huo ujao, hakuna mauti, hakuna huzuni, hakuna maradhi, hakuna uzee. Ee Mungu, yote yatakuwa ni mapya kule, kwenye ustaarabu Wako.

272 Mungu, tugeuze leo, kwa nguvu Zako, kwa kufanya upya nia zetu, tupate kuondokea vitu vidogo sana vya ulimwengu huu sasa, tuingie kwenye Neno la Mungu. Na jalia tufanywe upya kwa nguvu za kugeuza za Mungu juu ya Mbegu iliyo moyoni mwetu, kwamba tunaamini, tupate kuwa viumbe wanaoitwa wana na binti za Mungu. Haya ndiyo maombi yangu Kwako, Baba, kwa ajili ya watu, katika Jina la Yesu. Amina.

273 Sasa kwenu mlio huko nje kwenye matangazo, popote mlipo, ninawatakeni mumpokee Kristo huko nje, kama Mwokozi wenu binafsi, mkajazwe na Roho Wake. Maneno ambayo yamesemwa asubuhi ya leo, na yaingie moyoni mwenu. Na hapo umpokee Yesu. Nawe uyachunguze maisha yako, uone vile utakavyoishi baadaye. Na uchukue Chujio la mtu mwenye busara hapa. Ukijiona ukifanya jambo fulani ambalo ni kinyume na Neno hili, liondokee, upesi sana. Unaona? Kwa sababu, kuna Chujio linaloweka mauti mbali na wewe, hilo ni Neno la Mungu. Maneno Yake ni Uzima, nayo yatakukinga na mauti.

274 Ninyi watu hapa sasa mlio kwenye chumba hiki cha mikutano, nimewaweka hapa kwa muda mrefu. Ninawashukuru kwa kuja kwenu. Ninaomba ya kwamba Mungu kamwe hataiacha Mbegu hii ife. Natumaini hamuwazii ya kwamba ninasimama hapa kusema tu mambo haya nipate kuwa tofauti. Ninayasema kwa sababu ya upendo; na nikijua ya kwamba ni wakati nikiwa mwanadamu, kama nilivyo sasa, ndio wakati pekee nitakaoweza kuwahubiria watu. Nami ninampenda Yesu Kristo. Yeye ni Mwokozi wangu. Pia kumbukeni, ningekuwa huko nje mitaani kama isingalikuwa ni Yeye. Ningalikuwa huko nje; wazazi wangu wote, watu wangu wote, walikuwa ni wenye dhambi. Lakini Mungu, kwa nguvu Zake za kugeuza, ninajua zilinifanya kiumbe tofauti. Nami ninaweza—ninaweza kuwapendekezea, kwamba ni mwema. Naye atawalinda kwenye wakati wa shida. Hata kwenye mauti, mlangoni, hamna hofu. “Hakuna kitu kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu, ulio katika Kristo.” Mungu na ambariki kila mmoja wenu, na awape Uzima wa Milele.

275 Ni wangapi hapa ndani wasio na Mbegu ya Mungu, ubatizo wa Roho Mtakatifu? Waweza tu kuinua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham, kwamba nitampokea huyo Roho Mtakatifu." Sasa lichukue Neno mo—moyoni mwako, na uliamini. Sasa kama ukininii. . . Unaweza kujiangalia. Nenda ukajiangalie kwenye kioo, nawe unaweza kuona mahali ulipo. Unaona, unaweza kujua.

276 Unasema, "Vema, sikuinua mkono wangu, kwa kuwa ninaamini ninaye."

277 Jiangalie kwenye kioo, ndipo uone ni roho ya aina gani inayokudanganya, unaona. Mawazo ya udanganyifu! "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti." Hiyo ni kweli?

> Pale msalabani alipofia Mwokozi wangu,
> Hapo ambapo nililia nipate kusafishwa na dhambi;
> Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
> Utukufu. . .

278 Fumbeni tu macho yenu, kwa dakika moja sasa, na mumwimbie huo tu. Hebu na tuinue mikono yetu.

> Utukufu kwa Jina Lake, Jina Lake la thamani!
> Utukufu kwa Jina Lake!
> Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
> Utukufu. . . Lake.

279 Ninawatakeni ninyi Wakristo mpeane mikono, mliookoka.

> Nimeokolewa na dhambi kiajabu,
> Yesu anakaa ndani vizuri sana,
> Pale msalabani ambapo alinichukua;
> Utukufu kwa Jina Lake!
>
> Utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!
> Utukufu kwa Jina Lake!
> Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
> Utukufu kwa Jina Lake!

280 Ile Damu ina chembe hai ya Uzima ndani Yake, mwajua. Hii ni kwa hao wasiomjua.

> Loo, njoo kwenye Chemchemi hii ya fahari na nzuri;
> Itupe maskini nafsi yako miguuni pa Mwokozi;
> Loo, jitumbukize leo hii, na ufanywe mzima;
> Utukufu kwa Jina Lake!
>
> O, utukufu kwa. . .

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa tunapouimba.

> Utukufu kwa Jina Lake!
> Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
> Utukufu kwa Jina Lake!

281 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Paulo alisema, "Nitaimba katika Roho. Nitaabudu katika Roho." Na tuuimbe tena polepole sana, huku tumeinua mikono yetu.

282 Mnajua, shida yake, sisi Wapentekoste, tumepoteza furaha yetu, tumepoteza hisia zetu. Kama vile Billy Graham alivyosema hivi majuzi usiku, "Hao wahubiri, ukosi uliopinduliwa, wakishuka kwenda Kusini, wakipiga makofi yao, na wakienda kwa vishindo huku na huku ardhini, na kukanyaga-kanyaga kwa nguvu, walikuwa na kitu walichofurahia." Vema, naam, nina Kitu ninachofurahia. Mnaona? Mnaona? Naam. Naam, tumepoteza hisia yetu.

283 Sasa hebu na tuiinue tu mikono yetu. Usijali juu ya machozi, hayatadhuru kitu, mnaona. Hayo hayadhuru. "Yeye aendaye zake akipanda, akilia, hakika atarudi tena, akileta miganda ya thamani." Vema.

Utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!
Utukufu kwa Jina Lake!
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa . . . (Ee Mungu! Mungu asifiwe!)
Utukufu kwa Jina Lake!

Izamishe Mbegu, Bwana, moyoni!

Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

*Nguvu Za Mungu Za Kugeuza* SWA65-0911
(God's Power To Transform)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 11 Septemba, 1965, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Ramada huko Phoenix, Arizona, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org